Nipashe
Ijumaa Novemba 29, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580088
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Waziri Mbarawa kutoa ushahidi wa kesi wizi wa fedha mtandaoni

UKURASA 3


BUFE
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mbunge Maige adokeza wapi Veta inasimamia pengo ajira
Handeni inapogeuza maajabu na utajiri wake kuvutia watalii
UCHUMI
Habari katika picha
Kinamama Mafia 'hawajambo' kibiashara, tishio kuu usafiri Ukurasa 19

UKURASA 13

# Viribatumbo vyatafuna mabilioni bima ya afya

• **Vyatumia** asilimia 40 ya NHIF, Makinda ataja sababu kufuta kadi za vikundi... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WANAORUBUNI WENYE VVU WAHADHARISHWA**



WAGANGA wa jadi na baadhi ya wachungaji wa taasisi za dini wameshutumiwa kwa kuwarubuni watu wanaoishi...

## Mbinu kupaa uchumi EAC hizi
UKURASA 3




Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe (kulia), akiingia kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya uchochezi, inayomkabili pamoja na wenzake wanane. Kesi hiyo, ilishindwa kusikilizwa kwa kuwa mshtakiwa huyo, alikuwa na ahadi na daktari kwa ajili ya kuangalia afya yake. Kushoto ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store


## Wakurugenzi waliokopa benki biashara kitanzini

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAJIPANGA KUENDELEZA DOZI UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Miadi ya daktari yakwamisha kesi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeshindwa kusikiliza kesi ya uchochezi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, na wenzake wanane kwa kuwa mshtakiwa huyo ana ahadi na daktari kwa ajili ya kuangalia afya yake.

Madai hayo yalitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, wakati akiwasilisha nyaraka za daktari zikielekeza kwenda hospitali jana.

"Hali ya mshtakiwa bado si nzuri. Mheshimiwa hakimu, mshitakiwa alitakiwa kuonana na daktari saa 4;00 asubuhi ya leo (jana) lakini kwa kuheshimu amri ya Mahakama amelazimika kuomba daktari aahirishe muda ili afike kwenye kesi yake tunaomba kesi hii iendelee kuanzia Desemba 2-6, mwaka huu" alidai Kibatala.

Akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashitaka, Joseph Pande, alidai kuwa Kibatala aliomba ahirisho Novemba 26, mwaka huu, na kukubaliwa bila kuwapo maelezo ya miadi ya daktari, hivyo inashangaza kuona taarifa hizo zikiwasilishwa jana.

Pande alidai kama afya ya mshtakiwa ilikuwa bado haijakaa sawa na ana ahadi na daktari, ilitakiwa iwasilishwe Novemba 26, mwaka huu, au wakati wowote mapema kabla ya shauri hilo.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Mashtaka, Faraja Nchimbi, alidai aliomba mahakama iendelee na kesi hiyo kwa kufuata kifungu cha 147 cha sheria ya ushahidi sura ya tano kinachoruhusu mshitakiwa mwingine kuendelea na ushahidi.

"Mheshimiwa ikikupendeza niiombe mahakama ifuate kifungu cha 147 cha Sheria ya Ushahidi sura ya tano kinachoruhusu mahakama imruhusu mshtakiwa andelee na matibabu lakini iendelee kusikiliza ushahidi wa mshtakiwa mwingine," alidai Nchimbi.

Akitoa uamuzi baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Hakimu Simba alisema kesi hiyo ni ndefu na wasipokuwa makini haitaisha, hivyo akaaihirisha kwa siku ya jana tu kinyume cha maombi ya upande wa utetezi.

Kesi hiyo itasikilizwa tena leo saa nne na nusu asubuhi.

Novemba 26, mwaka huu, mahakama hiyo iliahirisha kesi hiyo hadi jana kwa madai kuwa hali ya afya ya Mbowe haikua nzuri na alihitaji kupumzika.

Mbali na Mbowe, washitakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashitaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, jijini Dar es Salaam.

# Viribatumbo vyatafuna mabilioni bima ya afya

**Na Romana Mallya**

MAGONJWA yatokanayo na viribatumbo yamekuwa yakigharimu mabilioni ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imeelezwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF, Anne Makinda, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua vifurushi vipya vya bima ya afya.

Vifurushi vilivyozinduliwa vimegawanywa katika makundi matatu yaliyopewa majina ya 'Ninajali Afya', 'Wekeza Afya' na 'Timiza Afya'.

Katika uzinduzi huo, Makinda aliyekuwa Spika wa Bunge la 10, alibainisha kuwa asilimia 40 ya fedha za mfuko huo zinatumika kugharamia matibabu ya magonjwa yatokanayo na viribatumbo.

Alisema wanawake na wanaume wanapaswa kuachana na kile alichokiita sifa unapokuwa na kiribatumbo, akieleza kuwa kina madhara makubwa kiafya.

"Taarifa tulizo nazo, wanasema katika wanawake 10, saba ni shida tu, ndiyo maana mnaanza presha, vidonda vya tumbo na mwisho wa siku unapata talaka kwa sababu hiyo, wewe kila siku unalala, kila wakitaka kukunyanyua mpaka wachukue winchi.

"Tujiimarisha kiafya, tuache utani zamani nilikuwa naona watu wa Afrika Kusini, Botswana na Swaziland wanawake walikuwa wakubwa, mwaka 1983 nikiwa waziri, nilipokwenda

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye akifungua kongamano la kuwajengea uwezo wahandisi nchini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakurugenzi waliokopa benki biashara kitanzini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ametoa siku saba kwa wakurugenzi wa halmashauri kuwasilisha taarifa za mikopo waliyochukua benki za biashara baada ya utaratibu huo kupigwa marufuku na serikali.

Jafo ameonya kuwa mkurugenzi yeyote atakayeshindwa kuwasilisha taarifa sahihi za mikopo hiyo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, waziri huyo alisema baada ya kuwasilishwa taarifa hizo, ofisi yake itafanya tathmini na ikibainika kuna mkopo ulichukuliwa na kuna sura ya shaka, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

"Tunataka mkurugenzi wa halmashauri awasilishe taarifa ya mikopo aliyochukua na kwa ajili gani, na riba yake ni kiasi gani, ndani ya wiki moja nipate taarifa katika halmashauri zote, sitegemei mkurugenzi yeyote afiche taarifa kuhusu halmashauri yake na endapo itabainika, hatua zitachukuliwa," alisema.

Waziri Jafo pia aliziagiza halmashauri zilizochukua mikopo hiyo na bado hazijaanza kuitumia, zirejeshe fedha hizo katika taasisi husika za kifedha zilikokopa.

"Wale ambao wameshachukua mikopo ndani ya wiki hiyo moja ambayo wameshatumia, walete taarifa Tamisemi mikopo hiyo ina sura gani, ilikuwaje na ofisi yangu itatoa maelekezo katika mikopo hiyo ambayo imechukuliwa,"alisema.

Jafo alisema kuanzia jana, kila kitu kinasimama kuhusu mambo ya mikopo kama ambavyo Waraka wa Serikali unaelekeza. "Halmashauri mbalimbali zimeonekana kuchukua mikopo kwenye benki za kibiashara kwa ajili ya miradi mbalimbali, jambo hili Rais jana (juzi) alilitolea maelekezo na alirejea kwamba halmashauri zilishaelekezwa kwa barua ya Desemba 13, 2016 yenye kumbukumbu namba CBC.155/233/01."

"Barua ilizitaka taasisi zote za serikali, zikiwamo mamlaka za serikali za mitaa, hazipaswi kuchukua mkopo wowote kutoka katika benki ya kibiashara hadi pale serikali itakapojiridhisha.

"Katibu Mkuu Hazina atajiridhisha kuhusu mkopo huo, lakini hapa katikati imeonekana kuna baadhi ya halmashauri kupitia mabaraza ya madiwani, wamekaa vikao na wanaamua kuchukua mikopo," alisema.

Alimwagiza Katibu Mkuu Tamisemi awasimamie wakurugenzi wake wote kuzingatia maelekezo ya serikali.

"Jambo hili halitavumilika, Katibu Mkuu ahakikishe wakurugenzi hawafanyi mambo kinyume cha maelekezo ya serikali.

"Kama vile jana mlivyoona Halmashauri ya Kahama, Jiji la Arusha walitaka kukopa kwa ajili ya stendi na tayari tumezuia tangu wiki iliyopita, na halmashauri zingine nataka watii maelekezo," aliagiza.

Waziri Jafo alisema baada ya tathmini ya taarifa hizo, atatoa taarifa ya halmashauri zitakazokuwa zimebainika kukopa bila kufuata utaratibu.

"Sasa, inawezekana walikuwa wana nia njema, lakini jambo hili ni kinyume cha taratibu na maelekezo ya serikali, kutokana na suala hili nimeamua kutoa maelekezo kwa halmashauri zote nchini kuwa hazipaswi kuchukua mikopo ya aina yeyote katika benki za kibiashara," alisema.

# HABARI KITAIFA



Mkazi wa Kijiji cha Dalai, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, Hashimu Kikwazi akinywesha maji mifugo yake kijijini hapo juzi. Hutozwa gharama ya Sh. 500 kwa kunywesha mfugo mmoja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kabudi aanika ukombozi kiuchumi Afrika Mashariki

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (pichani), amezishauri nchini wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kuimarisha umoja kwa maslahi ya watu wake.

Vilevile, mtaalamu huyo wa sheria amewashauri wafanyabiashara na wawekezaji wa nchi hizo kufanya biashara kwa maslahi ya uchumi wa wananchi wa jumuiya hiyo.

Prof. Kabudi alitoa ushauri huo jana jijini Arusha alipofungua Mkutano Mkuu wa Wafanyabiashara wa Afrika Mashariki na Wawekezaji katika kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

"Tunahitaji wafanyabishara wa Afrika Mashariki muwekeze katika biashara za kukuza uchumi wa kijamii kwa maslahi ya nchi hizi," Prof. Kabudi alisema.

Alizitolea mfano nchi za Ujerumani, Sweden, Denmark na Norway ambazo alidai wawekezaji na wafanyabishara wa sekta binafsi wamejikita katika uchumi wa kijamii ili kusaidia kukuza uchumi wa mataifa hayo.

Aliwataka wawekezaji hao kuachana na taratibu za nyuma na kuanza kuchukua hatua za kushirikiana kujikita kwenye biashara za kukuza uchumi wa kijamii zaidi ili kufikia lengo la kukuza uchumi wa mataifa hayo.

Katika mkutano huo, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Lubaret Mfumukeko, alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana katika miaka 20 tangu kuanzishwa kwa jumuiya hiyo, bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali.

Aliyataja matatizo hayo kuwa ni nchi wanachama kuwa na viwanda vichache, akifafanua kuwa ni kwa sababu ya kuwa na mitaji midogo ya kuanzisha viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Sekta Binafsi Tanzania, Godfrey Simbeye, alisema ubinafsi wa baadhi ya nchi wanachama wa EAC umesababisha biashara kutofanyika kwa kiwango kikubwa na kufaidisha wananchi.



Alidai baadhi ya nchi zimekuwa na ubinafsi kutokana na kununua bidhaa kutoka nchi za Ulaya ilhali bidhaa hizo pia zinazalishwa ndani ya jumuiya.

Simbeye alibainisha kuwa hadi sasa, ni asilimia 12 tu imefikiwa kwa biashara zinazofanyika kwa nchi zote sita EAC, jambo linalodidimiza kukua kwa biashara ya sekta binafsi kwa nchi hizo.

"Wenzetu wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU) wameshafikia asilimia 70 na wa Bara la Asia asilimia 50, sisi tusipoondoa ubinafsi na kujipendelea, safari ya kufika huko itatuchukua muda mrefu kufikia asilimia hizo," alisema.

**■Imeandikwa na Mary Geofrey na Daniel Sabuni (ARUSHA)**

## Waziri Mbarawa kutoa ushahidi kesi wizi wa fedha mtandaoni

**Na Hellen Mwango**

WAZIRI wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, anatarajia kutoa ushahidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi ya kesi inayomkabili mfanyabiashara Wilfred Massawe anayetuhumiwa kujipatia Sh. 700,000 kama rambirambi kwa kutumia jina la profesa huyo.

Massawe anakabiliwa na mashtaka manne ikiwamo ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kujifanya yeye ni Profesa Mbarawa (Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wakati huo). Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Salum Ally.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa alijitambulisha kwa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba, kwamba yeye ni Profesa Mbarawa anaomba fedha kwa ajili ya msiba.

Mapema mahakamani hapo, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, uliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa shahidi wa saba, Profesa Mbarawa.

Tayari upande wa Jamhuri umeita mashahidi sita akiwamo Mtendaji Mkuu wa TTLC, Kindamba.

Hakimu Ally alisema mahakama yake itaendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri Desemba 19, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Massawe anadaiwa Novemba 25, 2016 akiwa eneo la Yombo Buza, Temeke jijini Dar es Salaam, alijitambulisha kwa Alfred Samson kwamba yeye ni Profesa Makame Mbarawa.

Katika shtaka la pili, inadaiwa Novemba 26, mwaka na mahali hapo, Massawe alijitambulisha kwa Izack Mwawima kuwa yeye ni Profesa Mbarawa.

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la tatu, alijitambulisha kwa Waziri Kindamba kuwa yeye ni Profesa Mbarawa.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa Novemba 25, 2016 eneo la Yombo Buza Temeke, Massawe alijipatia Sh. 700,000 kutoka kwa Samson baada ya kujitambulisha kuwa yeye ni Profesa Mbarawa wakati huo akiwa Wizara ya Ujenzi akiomba fedha hizo kwa ajili ya kusaidia mazishi, huku akijua si kweli ni udanganyifu alioufanya kwa njia ya mtandao.


KDF Kilimanjaro Development Forum

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 688 591 182
john@stageneraltz.com
www.kilimanjarodevforum.co.tz

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANACHAMA**

Wanachama wa KDF wanatangaziwa kwamba kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama wote utakaofanyika tarehe 21, Desemba, 2019 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi.

**Agenda:**

1. Kupokea taarifa ya maendeleo ya KDF;
2. Kupokea na kupitia taarifa ya fedha ya KDF;
3. Kuchagua maafisa wa KDF na wajumbe wa bodi ya uongozi;
4. Kuteua wakaguzi na wadhamini au kuwathibitisha wanaoendelea;
5. Kupanga michango/ada za mwaka unaofuata, na
6. Kupitia na kupitisha marekebisho ya katiba.

**Uchaguzi wa viongozi katika nafasi zifuatazo;**

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Naibu Katibu
5. Mweka Hazina
6. Mweka Hazina Msaidizi

**Maombi ya kugombea nafasi hizi yatumwe kwa anwani zifuatazo:**
Dr. Jonas Kipokola,
Katibu (KDF),
S.L.P 8448, Moshi au barua pepe
info@kilimanjarodevelopmentforum.org au piga simu 0754386003
Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kugombea ni tarehe 7 Desemba, 2019.

Mkutano Mkuu utafuatiwa na sherehe ya Kilimanjaro Day itakayofanyika siku hiyo hiyo. Umoja wetu ndiyo nguvu ya mafanikio yetu, karibuni sana

**Imetolewa na:**
**Dr. Jonas Kipokola**
**Katibu, Kilimanjaro Development Forum**

61528802

# Wanaorubuni wenye VVU watahadharishwa

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

WAGANGA wa jadi na baadhi ya wachungaji wa taasisi za dini wameshutumiwa kwa kuwarubuni watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) kuacha kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV).

Ofisa Mawasiliano na Utetezi wa Mtandao wa Vijana wanaoishi na VVU Tanzania(NYP+), Humphrey Millinga, alidai hayo wakati akizungumza kwenye mdahalo uliohusisha taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya Ukimwi, uliofanyika, jijini hapa.

Mdahalo huo uliohusisha Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids), Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Tanzania (Nacopha), Mtandao wa Wanawake wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Tanzania (TNW), Mtandao wa Vijana wanaoishi na VVU Tanzania (NYP+) na UNAIDS, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yanayofanyika kitaifa jijini Mwanza na kilele chake kuwa Desemba Mosi.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Millinga alisema, waganga wa kienyeji huwapotosha wenye VVU kwa kuwaambia wamerogwa au kutupiwa majini na kuwataka waache kutumia ARV badala yake watumie dawa wanazowapa wao.

Pia alizituhumu baadhi ya taasisi za dini ambazo wachungaji wao huwaaminisha watu kuwa wanaweza kuwaombea na virusi vikaishi bila kutumia dawa. "Mara nyingi jamii ya waganga wa kienyeji imekuwa ikipotosha watu ikiwaambia labda acheni kutumia ARV, wakati mwingine anakuambia wewe hauna virusi bali umetupiwa jini hivyo anaambiwa aache dawa na apewe dawa za kumtoa huyo jini wakati huyo mtu anaacha dawa na anazidi kupata athari zaidi," alisema Millinga.

Alisema, mtu mwenye VVU njia pekee ya kupunguza makali ya virusi hivyo ni kutumia ARV kwa usahihi na kuiomba serikali kupitia Tacaids kuangalia suala hilo kwa undani zaidi.

Meneja mradi wa Nacopha, Agnes Godda, alisema kundi la waganga wa kienyeji limeachwa nyuma katika elimu ya mapambano ya VVU ambao wanatakiwa kuelimisha wateja wao na kuwahimiza kwenda hospitali kupima na kutumia ARV mtu anapokutwa na maambukizi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tacaids, Dk. Leonard Maboko, alisema tume yake imekuwa ikishirikiana na waganga wa kienyeji na kuahidi jitihada zaidi zinafanyika kuwahusisha viongozi wa dini kwa kuwa kupitia wao wanaweza kushawishi watu kutumia dawa vizuri na hata kupima.




Ofisa Uendelezaji Biashara wa Azania Group, Joel Laizer (kushoto), akikabidhiwa zawadi maalum na Mtangazaji wa EATV, Deogratius Kithama, baada ya kufanya mahojiano maalum na kituo hicho, jijini Dar es Salaam, katika mwendelezo wa kampeni ya EATV ya "Kibiashara Zaidi". **PICHA: EATV**

# Tume ya Haki Binadamu na Utawala Bora yaangukia vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, amesema tasnia ya habari kuwa ndio wadau wakubwa wa haki za binadamu nchini.

Jaji Mwaimu alisema hayo jana katika mkutano uliofanyika Zanzibar wa kuwajengea uelewa wa pamoja makamishna wa tume walioteuliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli.

Alisema katika kutekeleza jukumu walilopewa la kulinda, kuhifadhi na kutetea haki za binadamu nchini, wanawategemea sana vyombo vya habari kuelimisha jamii kuhusu haki zao.

"Vyombo vya habari ni wadau wetu wakubwa sana. Wao ndio waelimishaji, wao ndio wamekuwa wakati wote wakiibua matukio mbalimbali ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa lengo la kuujulisha au kuelimisha umma," alisema.

"Nyie ndio mtakaoitangaza tume. Kwa msingi huo, niseme kuwa tutaendelea kuwashirikisha katika yale yote tutakayokuwa tunayafanya ili kupitia ninyi wananchi watafahamu kuhusu tume inachokifanya," aliongeza.

Mwenyekiti huyo alisisitiza kuwa tume haiwezi kufanya kazi peke yake bila kushirikiana na wadau wengine kama vyombo vya habari, idara za serikali, asasi za kiraia na taasisi za kimataifa. "Ni lazima tujenge uhusiano mzuri wa kazi baina yetu. Hatuwezi kufanya kazi peke yetu, hivyo ni muhimu kufanya kazi na idara mbalimbali wakiwamo wadau wa maendeleo," alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi Zanzibar, Assaa Ahmad Rashid, ambaye alifungua mkutano huo, alimweleza Jaji Mwaimu kuwa dhamana waliyopewa ni kubwa kwa kuwa haki za binadamu ndio msingi katika nchi na kwamba wameaminiwa hivyo hawana budi kulitekeleza jukumu hilo kwa ufanisi ili kuwasaidia wananchi.

"Jukumu mlilopewa serikali ni kubwa. Tunawaahidi kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano katika kuifanya tume kutekeleza majukumu yake vizuri," alisema.

Rashid pia alisema kuteuliwa kwa viongozi hao kunatoa fursa kamili na ya wazi kwa mwananchi kupeleka malalamiko yake na kwamba serikali imejenga mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa wadau wote husan asasi za kiraia na wakati wote serikali itaendelea kushirikiana na taasisi zote zikiwamo za kimataifa ili kuhakikisha yale malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

"Tunatambua kuwa katika kutekeleza majukumu yenu kuna changamoto mnazo kutana nazo, ikiwamo uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki zao lakini mwendelee kueneza elimu hiyo kwa kushirikiana na taasisi zingine," alisema.

# Viongozi wa dini kupigia debe CHF

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIONGOZI wa dini wamewataka wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa) ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Askofu wa Kanisa la EAGT, Dk. Yohana Masinga, alisema hayo jana kwenye mkutano wa viongozi wa dini na mfuko huo mkoani hapa.

Dk. Masinga alisema viongozi wa dini wana wajibu wa kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa kadi za CHF.

Alisema viongozi wa dini wanakutana na jamii katika utoaji neno la Mungu, hivyo watatumia nafasi hiyo kuwaelimisha kuhusu kuwa na Bima ya CHF iliyoboreshwa.

Kwa upande wake, Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Shaaban, alisema CHF ni muhimu kwa jamii kwa kuwa itasaidia wananchi kupata matibabu kwa gharama nafuu.

Alisema serikali haijakosea kuwatumia viongozi wa dini kuhamasisha hilo na watahakikisha wanashirikiana ili wananchi wakate bima hiyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda, aliwaomba viongozi wa dini kuwasaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na maboresho hayo ili wananchi wajiunge.

Mukunda alisema serikali imeamua kushirikiana na viongozi wa dini kwa sababu ndio wanakutana na watu mara kwa mara katika mikusanyiko ya uhitaji wa huduma ya neno la Mungu.

"Tunaomba viongozi wa dini mtusaidie serikali katika hilo, tunahitaji kuona kila mwananchi anakuwa na kadi ya Bima ya Afya ya CHF," alisema Mukunda.

Alisema huduma hiyo hivi sasa imeboreshwa na wagonjwa wanatibiwa kwa gharama iliopangwa na mfuko huo isipokuwa kuna baadhi ya vipimo vikubwa ambavyo mgonjwa hawezi kupata.

Mratibu wa CHF Mkoa wa Dodoma, Dk. Francis Lutalala, alisema hivi sasa mfuko wa CHF umeboresha kwa kiasi kikubwa.

Alisema kwa sasa CHF ina akaunti katika kila mkoa ili wanachama wa mfuko huo wapate matibabu pale wanapofika katika mikoa mbalimbali.

Dk. Lutalala alisema kwa mwaka 2018 mkoa wa Dodoma ulikuwa na wanachama 1,463, lakini hadi sasa wamefikia 24,218.

## HABARI KITAIFA




Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na wananchi pamoja na watumishi wa shamba la miti la Buhindi, wakati akizindua bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari ya Ilenza, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza jana, ambalo limegharimu Sh. milioni 68 kutokana na mchango wa wadau wa shamba kwa kushirikiana na shamba hilo. **PICHA: WMU**

# Wajenga bweni kukabili mimba kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

KUONGEZEKA kwa idadi ya watoto wa kike kukatisha masomo kwa kupata mimba katika Shule ya Sekondari ya Ilenza wilayani Sengerema mkoani Mwanza, kumesababisha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wadau wa Shamba la Miti la Buhindi, kujenga bweni ili kuondokana na tatizo hilo.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa bweni hilo lililogharimu Sh. milioni 68, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, aliipongeza TFS na wadau wa shamba hilo kwa kuwa mstari wa mbele wa kuisaidia serikali kupunguza tatizo la ujauzito kwa watoto shuleni.

Sambamba na ujenzi huo, wadau hao wamejenga vyoo, bafu, uzio, umeme na kuchangia vitanda 24 kwa ajili ya watoto hao wa kike.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka kwa Mkuu wa Shule hiyo, Godson Antony, watoto wa kike wapatao 50 kila mwaka hukatiza masomo kutokana na ujauzito.

Antony alisema ujenzi wa bweni hilo utasaidia watoto wa kike kufikia malengo yao na kuepukana na vishawishi mbalimbali.

Aidha, Kanyasu alisema ujenzi wa bweni hilo utasaidia kupunguza utoro kwa watoto wa kike na kupunguza kutembea umbali mrefu kufika shule.

Kutokana na hali hiyo, Kanyasu aliutaka uongozi wa shamba hilo la miti kuendelea kuzisaidia shule zingine zinazopakana na shamba hilo hali itakayosababisha jamii hiyo kuona faida ya uwapo wa shamba hilo.

"Tutahakikisha pesa za ujirani mwema zinatumika kujenga mabweni katika kata zote zinazozunguka shamba la miti la Buhindi ili jamii kuona faida ya moja kwa moja ya uwapo wa msitu huo.

Aidha, Naibu Waziri Kanyasu aliuagiza uongozi wa shamba hilo kuweka miundombinu ya maji katika shule kupitia fedha za ujirani mwema ili kupunguza tatizo la watoto wa kike watakaokuwa wakiishi katika bweni hilo kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kuchota maji.

Naye Meneja wa Shamba hilo, Mussa Tinda, ambaye ni mwenyekiti wa mfuko ulioanzishwa na wavunaji wa kumtaka kila mteja anayepata fursa ya kupewa kibali cha uvunaji kuchangia 1,000 kwa mita za ujazo wa magogo anayouziwa, alisema ujenzi wa bweni hilo ni mchango kwa jamii ili kuwafanya watoto wa kike kutimiza ndoto zao.

Amesema mchango huu ni matokeo ya mafanikio na uhusiano mzuri uliopo katika jamii na watumishi wa shamba hilo.

# Waangalizi watoa neno uchaguzi mitaa

**Na Elizabeth Zaya**

WAANGALIZI wa uchaguzi kutoka katika Taasisi ya Tafeyoco iliyofanya uangalizi katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, imetoa tathmini ya uchaguzi wa serikali za mitaa huku ikisema ulikuwa huru na haki.

Pia imesema imebaini baadhi ya changamoto zilizochangia baadhi ya wagombea kuenguliwa katika uchaguzi huo ni kushindwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi katika ujazaji wa fomu za kugombea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tafeyoco, Elvic Makumbo, alisema wagombea wengi waliacha kufuata taratibu za uchaguzi na kufanya mazoea, hivyo kujikuta wakifanya makosa ambayo waliona ni madogo ambayo kisheria na kikanuni hayakubaliki.

"Unajua watu wana mazoea sana. Tumebaini kwamba watu walichukua fomu na kwenda kujifungia ndani kuanza kujaza bila hata kuzingatia kwamba kuna kufuata masharti na maelekezo. Kwa hiyo walikuwa wanajijazia tu ovyo, mtu badala ya kujaza kirefu anajaza kwa kifupi," alisema Makumbo na kuongeza: "Kwa mfano badala ya kujaza Chama Cha Mapinduzi (CCM), anajaza kifupi chake wakati kisheria anakuwa amekosea na tumegundua kwamba kilichowaondoa wengi ndiyo hicho kufanya makosa ambayo waliona ni madogo."

Alisema walibaini kwamba wagombea wengi walikosea kutokana na baadhi ya vyama vyao kushindwa kuwapatia elimu ya uzingatiaji wa sheria na kanuni hizo za uchaguzi.

"Pia tumebaini kwamba baadhi ya vyama havikutumia muda mwingi kuandaa wanachama wao hasa wagombea katika kujua sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi na hii ilichangia wengi wakose sifa," alisema. Kuhusu baadhi ya vyama vya siasa kutangaza kutoshiriki katika uchaguzi huo, Makumbo alisema wamegundua kwamba viongozi wa vyama vilivyojitoa katika uchaguzi huo vilifanya uamuzi huo bila kuwashirikisha wala kuwaelewesha wanachama wao wa chini, hivyo kuacha malalamiko na huzuni kwa wagombea wengi.

"Tumekumbana na malalamiko mengi kutoka kwa wanachama hususani wa vyama vya upinzani vilivyojitoa, wanasema wagombea wengi walikuwa wanakubalika, lakini uamuzi wa viongozi wao wa juu umewaathiri, wanalalamika na wanahuzunika," alisema Makumbo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Miradi nyumba za kuuza izingatie gharama halisi

**KATIKA** kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata makazi bora na yenye gharama nafuu, serikali imeshusha bei za nyumba za miradi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) nchi nzima kwa karibu asilimia 50 baada ya kubaini zinauzwa kwa gharama kubwa na Watanzania kushindwa kumudu kuzinunua.

Nyumba za vyumba viwili vya kawaida zilizokuwa zinauzwa kwa Sh. milioni 66 zimeshushwa hadi Sh. milioni 36.58 wakati nyumba 169 zenye vyumba vitatu vya kawaida zilizokuwa zinauzwa kwa Sh. million 67.26, Mthamini Mkuu wa Serikali amesema zinaweza kuuzwa kwa Sh. milioni 35 pamoja na kodi ya Sh. 6,300,000, zitauzwa kwa Sh. milioni 41.3.

Pia nyumba 146 zenye vyumba vitatu, viwili vya kawaida na 'master bedroom' zilizokuwa zinauzwa Sh. milioni 74.34 zitauzwa hadi Sh. milioni 39 pamoja na kodi ya Sh. 7,020,000 sasa zitauzwa Sh. milioni 46.02.

Nyumba yenye vyumba vitatu na 'master bedroom' iliyokuwa inauzwa Sh. milioni 83.78 sasa itanunuliwa kwa Sh. milioni 52 pamoja na kodi ya Sh. 9,360,000 itauzwa kwa Sh. milioni 61.36.

Uamuzi huo ulitangazwa juzi jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, alipohitimisha kutembelea miradi ya PSSSF.

Mradi huo wenye nyumba za gharama nafuu katika eneo la Buyuni, Chanika una nyumba 480 kati ya hizo 204 hazijapata wanunuzi na 276 malipo yake hayajakamilika.

Waziri alisema mdororo wa ununuzi wa nyumba hizo umesababishwa na makato ya urejeshwaji ya kila mwezi kuwa juu na watumishi wengi kutokumudu bei za nyumba hizo, huku akisema lengo la kujenga nyumba hizo ni kuwauzia watumishi na Watanzania kwa bei nafuu na badala ya kukaa nazo.

Alisema menejimenti ya mfuko iliridhia kutumia Mtathmini Mkuu wa Serikali ili kupata tathmini na thamani halisi ya nyumba hizo kuwa bei halisi na soko lililopo.

Uamuzi wa kushusha bei hiyo kwa nusu ya gharama unaashiria kuwa mchakato kujenga na kuuza nyumba hizo ilikuwa na mapungufu kwa sababu wahusika walipaswa kufanya utafiti wa kina, ikiwamo kuangalia uwezo wa watumishi, wanancni na bei ya soko la nyumba nchini.

Hili linadhihirishwa na Mhagama mwenyewe kwa kueleza kuwa gharama hizo zilikuwa zinawaumiza wananchi, wakati nia ya serikali ni kuwasaidia wananchi wake.

Bila kufanya maandalizi ya kutosha sambamba na utafiti wa kina, miradi ya ujenzi wa nyumba za kuuza itaendelea kuwa mzigo kwa serikali na taasisi zake kwa kuwa nyumba hizo zitakuwa zinajengwa na kukosa wanunuzi kutokana na bei yake kutoendana na uwezo wa watumishi na wananchi kwa ujumla wake.

Kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanapata makazi bora na kwa gharama nafuu, basi hakuna sababu ya kuzijenga na kuziuza kwa bei ambayo hawataweza kuimudu.

Hata hivyo, suala la makazi bado kina mahitaji makubwa kwa wananchi wengi wanaoishi mijini bila kujali kuwa mhusika mfanyakazi au la, hivyo serikali na taasisi zake bado utekelezaji wa miradi ya nyumba ni fursa ya kuingiza mapato.

Ushauri wetu ni kuwa miradi ya ujenzi wa nyumba za kuuza kwa watumishi wa serikali na Watanzania kwa ujumla iendelee kutekelezwa, lakini zijengwe nyumba ambazo gharama zake wengi wataweza kuzimudu.

Miradi ya aina hii inaweza kuelekezwa zaidi kwa Jiji la Dodoma ambalo limekuwa makao makuu ya nchi, hivyo kuwa na watumishi wote wa umma na ongezeko zaidi la watu, huku jambo la msingi ilikuwa umakini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunapovunja sheria hivi tunategemea nini?

Na Yasmine Protace

**SHERIA** inapotungwa mahali popote ni wajibu wa kila mtu kuzifuata. Mtu anayevunja sheria kwa makusudi, anastahili kuchukuliwa hatua.

Kutungwa kwa sheria, lengo lake ni kuwataka watu wazitii, ili zilete manufaa katika eneo husika.

Mara nyingi, kuna makundi katika jamii yamekuwa yakiibuka kukaidi hata maelekezo wanayopewa na ama viongozi au serikali. Inachangia kuangukia uvunjaji wa sheria.

Linalotakiwa ni kwamba, kila mtu anapaswa kufuata sheria, jambo litakapomfanya aanguke katika kuvunjwa sheria za nchi, ambazo kila mtu anapozifuata, hakuna shaka anakuwa mbali na changamoto hizo.

Inawezekana, baadhi yetu hatuzijui kwa undani sheria zilizopo na kusababisha umma kuangukia katika ukiukwaji wake.

Nianze na hili ambalo lipo katika baadhi ya ofisi za serikali na panapopatikana huduma zake, zikiwamo picha zinazoelekeza uvaaji nguo. Mgonjwa anayefuata huduma anapaswa kuvaa nguo zenye maadili, akikiuka unarudishwa nje.

> **Nianze na hili ambalo lipo katika baadhi ya ofisi za serikali na panapopatikana huduma zake, zikiwamo picha zinazoelekeza uvaaji nguo. Mgonjwa anayefuata huduma anapaswa kuvaa nguo zenye maadili, akikiuka unarudishwa nje**

Inawezekana mhusika hakulijua hilo na anapokutana na zuio ndipo linamfungua umevunja sheria za nchi. Hapo inaanza kumpa maswali binafsi, kinachofanya mpaka kuvunja sheria za nchi na baadhi ya sehemu za mjumuiko ni nini?

Kuna nilichokiona hapo katika hospitali kubwa jijini Mwanza, ambako pia kuna chuo cha madaktari na wengine wa fani ya tiba, inashangaza mantiki yake.

Hapo kuna kozi mbalimbali zinazotolewa mahali hapo na kila mwaka kuna wanaofuzu mafunzo hayo ya tiba, huku kukiwapo orodha nyingine kubwa ya wanaochukua nafasi kujiunga na mafunzo.

Katika chuo hicho, ndiko kuna geti linalotumiwa na wanachuo kuingia. Ni mahali kunakopatikana na katazo kuingia na nguo zisizofaa kimaadili, ama kwenda kupata matibabu au mahitaji mengineyo ndani ya mazingira hayo. Inawahusu pia wanachuo na wadau wake wote.

Katika geti hilo kunakatazwa kuingia na nguo zisizo na maadili. Nimeshangaza, kuona baadhi ya vijana hawazingatii hilo na wamekuwa wakigombana na walinzi kutokana na kuvaa nguo zisizo na maadili.

Vijana hao wanakatazwa kuingia hospitali kutokana na kuvaa nguo zisizo na maadili, lakini huwa nawashuhudia wanakuwa wakali na wameonewa kurudishwa nje ya geti.

Nilishuhudia malumbano, baadhi ya wanachuo waliporudishwa nje kutokana na nguo walizovaa, walidai nguo walizovaa 'matilio' yake inapanda juu na ndio maana zinaonekana fupi.

Mmoja wao, anayefanya kazi katika hospitali hiyo, anasema watoto wengi wanaharibika kutokana na malezi.

Anasema matangazo yapo, lakini wanayapuuzia na kuendelea kuvaa nguo zisizo na maadili.

BARUA & MJADALA

# Tukague biashara za injini 'used'

**Mhariri,**

*KWELI nikiri tuko katika biashara huria kitaifa, na hili tumelianza tangu mwaka 1985, mlango wa uhuria kufungiliwa tangu ufungwe mwaka 1964.*

*Hilo halina la kujadili kuhusiana na mageuzi yanayotokea, Shida yangu ni kuona namna utitiri wa vyombo na mashine zilizotumika zikijaa kila mahali mitaani.*

*Huwa inanipa tabu, kwani tulianza kuona vifaa kama mitumba kwenye kompyuta na mashine ndogo. Kadri siku zinavyoenda, sasa kuna mitaa hasa ya jijini Dar es Salaam, nashangaa kuona injini nyingi za magari zinauzwa, baadhi zinatoa maswali .*

*Je hii ni salama na tumefikia hatua hiyo? Nadhani katika mfumo wa kiusimamizi kiserikali tuna vyombo vya kutosha kufanya kazi hiyo. Kwa mfano, kuna kila sababu kukawapo ufuatiliaji wa kitaalamu, kujua usahihi na uthabiti wa hayo kwa maendeo yetu.*

*Nadhani huko nyuma, mamlaka ya juu kiserikali mara moja au mbili, ilishatoa kauli za tahadhari 'soko huria pasipo usimamizi inakuwa soko holela.'*

*Ni mtazamo unaoweza kusogezwa katika mustakabali mpana zaidi katika hayo ninayoongea na nimaamini kunapofanyika ufuatiliaji wa kina kuna mengi ya kuibuliwa huko.*

*Si mbaya kama mamlaka husika kama vile Shirika la Viwango la Taifa (NBS) zikakutana wadau wenzake kujadilii na kushirikiana na wataalamu kutoka vyuo, kama vile chuo cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT) kutafuta majibu sahihi.*

**Ebus Makidi,**
**Dar es Salaam,**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Tunza barabara nayo ikutunze, kuihujumu ni uhalifu kwa taifa




**Na Peter Orwa**

**NISEME** Tanzania kama ilivyo nchi yoyote ya dunia ya tatu, ni kwamba miradi ya barabara ni 'roho yake' ambayo inaendelea kuumbwa kila kukicha.

Tangu 'Uhuru mchanga' bandari ya Dar es Salaam ikifanya kazi yake, zama ambazo shaba ilichimbwa kwa wingi kutoka majirani wa Zambia, barabara kati ya Dar es Salaam na mpakani Tunduma ilifanyiwa kazi kubwa.

Waliokuwapo na wanaofuatilia historia wanajua namna gani safari za malori hasa aina ya Fiat na tela zao yakipatia kubeba mizigo hiyo hata jina 'Magomeni Mapipa' ikazaliwa jijini Dar es Salaam.

Wakazi wa miji ya barabarani kama vile Chalinze Pwani, Mikumi na Morogoro mjini, Ilula na Nyololo Iringa na Igurusi Mbeya wana simulizi kamili za kihistoria.

Ikifuatiliwa tangu zama hizo hadi leo hii, serikali imewajibika vilivyo katika hatua mbalimbali za kuilinda barabara hiyo, ikiwamo matengenezo baada ya ujenzi huo wa mwanzo. Ushahidi ni mlima Kitonga, Iringa.

Miaka ya baadaye, zama za 1980 safari ngumu kati ya mji makao makuu ya kitovu cha wazalishaji mahindi Songea, Mkoa wa Ruvuma na Makambako kupitia Njombe, nako kukazinduliwa barabara, zao la wajenzi kutoka kampuni ya Balfour Beatty. Jijini Dar es Salaam, kampuni ya Mowlem ikajenga barabara mpya kuunganisha bandarini na Ubungo, Port Access Road mwaka 1979, ambayo baadaye ikabatizwa upya Nelson Mandela Road, kuwapokea wabeba shaba kutoka barabara ya Morogoro.

Hadi leo hii watu wanajivunia matunda hayo. Hicho ndichi katika miaka ya 1990 kukafanyika katika barabara ya kuuganisha mkoa wa Mtwara kulikosahaulika kwa muda mrefu na Dar es Salaam. Hatimaye kazi ilifanyika, leo hii kunafikika kwa 'kuteleza.'

Linaenda mbali zaidi, katika miaka ya katikati kuanzia mwaka 2006, kazi ya Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete kuunganisha Masasi na Tunduru, pia kutoka mahali hapo na Songea, kupitia Namtumbo.

Maana yake ni nini na mifano hiyo ya kina kihistoria? Kuzipata barabara hizo ni tabu, ikitujengea maana ya kuwapo wajibu mkubwa wa kuzilinda. Kama hujui shida hiyo, waulize wakazi wa Mtwara na Songea wakufungulie 'CD' kamili.

Nakumbuka kuna wakati serikali ya Ujerumani ilichukua hatua ya kuboresha barabara, ikafanyia kazi ya kuboresha barabara kati ya Mombo na Lushoto.

Kubukumbu katika tukio la makabidhiano wafadhili walisisitiza utunzaji, hasa wakigusia wao kuhusika na ujenzi wa barabara ya mwanzo miaka mingi sana iliyopita.

Huo ni ujumbe ambao tunapaswa kuzingatia mithili ya matunzo ya mboni ya macho yetu kama waswahili wanavyotamka 'usione vyaelea vimeumbwa.'

Mipango na michoro ya barabara leo hii, ukienda kwa kina ni zao la mikakati, baadhi naikumbuka katikati ya miaka ya 1980, Waziri aliyehusika na Ujenzi, Nalaila Kiula, alianzisha kupitia alichokiita 'Integrated Road Project.' Kumaanisha hoja ya kuwa na michoro kunganisha barabara kitaifa.

Sote tunakumbuka kazi ya Rais John Magufuli, wakati huo alikuwa waziri mwenye dhamana na barabara. Kama hali ndiyo hiyo, tunapaswa kujiuliza kama hatua kama hizo zinachukuliwa, kuanzia barabara zilizo chini Wakala wa Barabara Tanzania na katika ngazi za Halmashauri kupitia Tarura.

Pia, historia inaturejesha kulekule tulikokuwa, tukiwa na vyombo vya ujenzi serikali kama vile Comwoks wakati ule na RRM, yaani Rural Road Maintenance.

Tunaweza kujadili mengi ya kihistoria, lakini ujumbe mkuu ni wajibu wa kuthamini kutunza barabara. Hizi ni nyenzo za msaada na maendeleo.

Wajibu huo, hauishii kwa mtu mmoja mmoja, bali hata watendaji wa kiserikali kama vile katika halmashauri. Kuendesha kilimo jirani na kingo za daraja au kupitisha gari la mizigo mizito zaidi ya uzani unaotakiwa katika barabara husika, yote hayo yanaangukia uhalifu wa mali ya taifa. Kimsingi, tunza barabara nayo ikutunze.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Ubinafsi wakwamisha biashara EAC

Na Daniel Sabuni,
ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Godfrey Simbeye, amesema Ubinafsi wa baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) umesababisha biashara kutofanyika kwa kiwango cha mafanikio.

Akizungumza kwenye mkutano wa pili wa tathmini kwa wafanyabiashara wa nchi wanachama wa EAC jana jijini hapa, ulioandaliwa na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), alisema baadhi ya nchi zimekuwa na ubinafsi kwa kununua bidhaa kutoka Ulaya jambo linalofanya bidhaa za EAC kudorora.

"Mfano utakuta kuna nchi inaagiza bidhaa kama nguo kutoka Ulaya ambazo zinapatikana hapa hapa kwetu. Matokeo yake viwanda hukosa masoko na hata kufa na kupunguza ajira kwa wananchi wetu," alisema.

Simbeye alisema hadi sasa ni asilimia 12 tu ambazo zimefikiwa kwa biashara zinazofanyika kwa nchi zote sita wanachama wa EAC jambo ambalo linadidimiza kukua kwa biashara.

"Wenzetu wa Umoja wa Ulaya (EU) wameshafikia asilimia 70 na wa Bara la Asia asilimia 50. Tusipoondoa ubinafsi na kujipendelea safari ya kufika huko itatuchukua muda mrefu. Biashara inataka ushirikiano na kununua bidhaa kwa ushirikiano ili mradi ziwe na ubora," alisema. Aidha, Simbeye alisema inabidi wafanyabiashara wa nchi wanachama wajiulize maswali magumu kilichosababisha kuwafikisha kwenye asilimia 12 ni nini na hatua gani zichukuliwe. Alisema nchi za EAC hazina budi kuondoa vikwazo vya biashara kwa mfano bidhaa ikitoka nchi moja kwenda nyingine isizuiwe kwa maana kama kuna mfumo wa viwango wa pamoja ili kurahisisha bidhaa kuwahi sokoni na kuwaletea wafanyabiashara tija na kupunguza umaskini katika mnyororo wa faida kwa wananchi.

Alitoa mfano wa ushirikiano wa jumuiya utakaorahisisha na kufanikisha uwezeshaji wa wafanyabiashara wa Afrika Mashariki kufikia malengo kuwa na bei nafuu kwenye usafiri wa anga kwa nchi wanachama ili kurahisisha mwingiliano wa kibiashara na bidhaa na kuleta tija.

"Mfano unawezakuta nauli ya ndege kutoka nchi moja kwenda nyingine ni dola 450, wakati kwenda Mumbai nchini India ni 350. Hii inakwamisha wafanyabiashara wetu," alisema.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema serikali imejipanga kutoa ushirikiano wa kutosha kwa sekta binafsi na kuweka mazingira mazuri kibiashara ili kuungana na malengo ya wafanyabiashara wa jumuiya kufikiwa na kupunguza umaskini kwa wananchi wake.




Wananchi wakiangalia ajali ya lori na daladala katika eneo la Temboni Mbezi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenyeviti wapya waonywa kuhusu migogoro

Na Peter Mkwavila,
DODOMA

WENYEVITI wapya wa serikali za mitaa katika Jiji la Dodoma, wameonywa kutotumia madaraka yao vibaya na kuwa chanzo cha migogoro na wananchi.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkurugenzi wa Jiji, Godwin Kunambi, alipokuwa akizungumza na wenyeviti na wajumbe wa serikali za mitaa waliochaguliwa hivi karibuni baada ya kuapishwa.

Aliwataka kutotumia nafasi zao hizo kama sehemu ya kujipatia fedha kutokana na kesi wanazoamua bali wawatumikie wananchi bila kujali tofauti za kiitikadi za kisiasa.

Alisema nafasi walizochaguliwa zikatumike kwa ajili ya kutatua changamato za wananchi na siyo kuwa vyanzo vya kuongeza migogoro inayotokea kwenye maeneo yao.

"Mmethaminiwa na wananchi wenu kwa kuwachagua kushika nafasi hizo kwenu. Nikiwa mkurugenzi wenu, nina amini mtakuwa kielelezo katika kuhakikisha migogoro haitokea kwenye maneo yenu na pia nina imani mtakuwa mstari wa mbele kuimaliza ninyi wenyewe," alisema.

Pia aliwataka kuhakikisha wanasimamia shughuli za kimaendeleo kwa mujibu wa katiba na kanuni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuzingatia kuwa wao ni sehemu ya wasimamizi.

Alisema ili kufanikiwa katika kazi hiyo, wanatakiwa kushirikiana na watendaji wa kata na mitaa kwa kuwa wao ndio wataalamu katika shughuli za kiserikali na hata kwa jamii.

Awali, akizungumza baada ya kuwaapisha wenyeviti na wajumbe wao,

Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Dodoma, Paschal Mayumba, alisema kiapo walichokula ni kwa ajili ya uaminifu katika kuitumikia serikali na wananchi wakiwa viongozi waliaminiwa.

"Mmeapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na serikali tukufu na sio vinginevyo. Mkahakikishe mnadumisha amani kwenye maeneo yenu ikiwa na pamoja na kutatua changamoto za wananchi," alisema.

# Viribatumbo vyatafuna mabilioni bima ya afya

INATOKA UK. 2

Botswana kutafuta nguo, nililazimika kwenda kwenye duka la watoto maana kwenye maduka ya nguo za wakubwa hakuna 'size' (kiwango) yangu," alisema.

Makinda alisema nchi hiyo kwa sasa imepiga hatua kubwa kukabiliana na kiribatumbo, lakini anashangaa kuona tatizo hilo linamea nchini.

"Kimetokea kitu kama siyo kampeni sijui, sasa hali hiyo imehamia Tanzania, asilimia 40 ya mfuko (NHIF) inalipa gharama za mambo hayo, sasa inawezekana hiyo jamani?" Alihoji.

Makinda alisema ameamua kuyasema hayo kwa sababu kiribatumbo ni kifo, akieleza kuwa kunywa pombe au nyama si dawa.

"Unachukua rafiki zako mbuzi mzima, wawili au watatu mnawamaliza, tujiangalie, hili tatizo siyo utani," alisema.

Makinda pia alitaja sababu ya kufutwa kwa Bima ya Afya ya Vikundi (Kikoa), akieleza kuwa wamebaini waliokuwa wanajiunga, asilimia 90 walikuwa ni wagonjwa.

"Watu wanajiunga pamoja ili wapate bima za afya, lakini kumbe walikuwa wanawachangia wenzao wagonjwa, tuligundua Vikoa asilimia 90 ya wajumbe walikuwa wagonjwa, kama mfuko tukaona tunakufa," alisema.

Makinda alisema ili kuwezesha kila Mtanzania kukata bima ya afya, wameamua badala ya kukaa ofisini, watawafikia majumbani, makanisani, misikitini na mitaani.

Pia aliwataka watoa huduma kuhakikisha wanatoa huduma bora na waache kutoa hesabu za uongo au dawa zilizovuka muda wa matumizi.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema vifurushi hivyo ni mpango wa hiari, akiwahimiza wananchi kujiunga kwa faida yao.

"Tumejadiliana na taasisi za fedha ili kuona kama kutakuwa na uwezekano mtu anayetaka kupata bima, basi alipe kidogo kidogo na atakapomaliza akabidhiwe, hili tutalifanya pia kwa kampuni za simu," alisema.

"Napenda kusisitiza kuwa, ukipata bima ya afya ili kuanza matibabu lazima ukae siku 30 ndipo uanze kupata huduma. Kwa muda wa wiki tatu za uhamasishaji, tumefanikiwa kupata wanachama zaidi ya 700," alisema.

Katika uzinduzi huo, baadhi ya wananchi walikabidhiwa kadi zao mpya wakiwamo wanachama wapya baada ya kuhamasika na vifurushi hivyo vipya.

HABARI KITAIFA

# Kanzidata ya Taifa ya DNA mbioni

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), ipo katika hatua za awali za uanzishwaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu (DNA) kwa ajili ya kuhifadhi taarifa zinazohusiana na makosa ya jinai.

GCLA watashirikiana na taasisi mbalimbali za umma zikiwamo Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Wakala wa Usajili na Ufilisi (Rita) na wataalamu wake watashirikishwa katika hatua za awali za uanzishwaji wa kanzidata ya taifa hususani utayarishaji wa andiko wa dhana la uanzishwaji wa kanzidata (concept note).

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya utendaji kazi wa mamlaka hiyo kwa miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Dk. Mafumiko alisema lengo la kuanzisha kanzidata ni kuongeza ufanisi katika kuboresha mazingira ya biashara kwa mamlaka hiyo.

Alisema uanzishwaji wa kazidata hiyo utazingatia ushauri wa wataalamu katika andiko la uanzishwaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu (concept note) na mamlaka inakusudia kuanza kuingiza taarifa zinazohusiana na makosa ya jinai.

"Kutokana na taarifa hizi kuwa zinahitajika katika utambuzi wa binadamu kwa ajili ya utatuzi wa changamoto mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa makosa ya jinai kama vile ubakaji, wizi, mauaji, majanga na masuala ya kijamii yakiwamo mirathi, uhalali wa mzazi kwa mtoto tumeona ni vema kuanzisha kazidata hiyo," alisema Dk. Mafumiko.

Aidha, alisema kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wamefuta jumla ya tozo 17 na kupunguza tozo nane katika utekelezaji wa Sheria ya Kemikali nchini.

Alisema kutokana na kupunguza kwa tozo hiyo katika Sheria ya Kemikali pia itaweza kupunguza mzigo wa gharama kwa wafanyabiashara wa kemikali katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Dk. Mafumiko alisema mamlaka imefanya pia marekebisho ya Sheria ya Kemikali za Viwandani na Majumbani Namba 3 ya Mwaka 2003 kwa kufanya maboresho ya kifungu cha 43(11) ili kuruhusu uingizaji wa kemikali katika ujazo mkubwa usiokuwa kwenye vifungashio (bulk).

"Marekebisho haya yanatarajiwa kuongeza wingi wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, Tanga au Mtwara kutegemeana na ipi itakuwa inatekeleza jukumu hilo na hivyo kukuza biashara na kuongeza mapato," alisema Dk. Mafumiko.

Kadhalika, alisema mapato ya mamlaka hiyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 9.342 kwa mwaka wa fedha 2015/16 na kufikia Sh. bilioni 24.246 sawa na asilimia 118 ya ongezeko la mapato kwa miaka minne.

Alisema sababu za kuongezeka kwa mapato hayo ni kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti na ukusanyaji wa mapato na kuimarika kwa mifumo ya ndani ya ukaguzi na udhibiti fedha kuimarika kwa utunzaji wa hesabu.

"Fedha hizi zimesaidia katika ununuzi na ukarabati wa mitambo ya maabara, kuboresha miundombinu ya maabara, kununua vitendanishi na kuimarisha ukaguzi wa kemikali," alisema Dk. Mafumiko.



Timu ya wajumbe kutoka Manispaa za Dar es Salaam, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Benki ya Dunia (WB), wakikagua mradi wa upanuzi na ujenzi wa kingo za Mto Ng'ombe, unaotekelezwa kupitia Mradi wa DMDP, chini ya fedha za mkopo nafuu wa benki hiyo, katika eneo la mpaka wa Kijitonyama na Tandale uzuri jijini humo, juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri amwagiza IGP kutumbua mkuu chuo

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni amemwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, kumwondoa Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi, Kamishna Msaidizi, Anthony Rutashuburugu, katika nafasi hiyo na kumshusha cheo kimoja. Masauni alitoa agizo hilo jijini Dar es Salaam baada ya mkuu huyo kukaidi maelekezo ya kuokoa kiasi cha Sh. 210,085,000 katika mradi wa ujenzi wa mabweni na madarasa chuoni hapo.

Naibu Waziri huyo alitoa maagizo hayo alipotembelea mradi wa ujenzi wa mabweni na madarasa ya chuo hicho, baada ya chuo kupokea Sh. milioni 700 kutoka kwa Rais John Magufuli.

Awali, Mhandisi Masauni alimwelekeza Mkuu huyo achukue hatua ya kuokoa fedha hizo kwa kuwatumia wafungwa ili waweze kufanya kazi katika mradi huo wa Chuo cha Taaluma ya Polisi kilichopo Kurasini jijini Dar es Salaam.

Alisema wizara ina taasisi ya magereza ambayo ina nguvu kazi ya kutosha. "Rais alishaagiza wafungwa watumike katika shughuli za uzalishaji, sioni sababu ya kutumia kiasi hicho cha fedha kuwalipa vibarua wa nje hivyo naagiza muwasiliane na Jeshi la Magereza pamoja na kikosi cha ufundi kilichopo ndani ya Jeshi la Polisi ili muweze kuona ni vipi mnaokoa kiasi hicho," alisema.

Akitoa taarifa ya awali ya ujenzi huo, Mkuu wa Chuo hicho, Naibu Kamishna Rutashuburugu, alisema majengo yatakayojengwa ni ghala la chuo, madarasa matatu, bweni moja la askari wa kiume na bweni lingine la askari wa kike.

# Rushwa ngono tishio kazini sekta binafsi

**Na Elizabeth Zaya**

RUSHWA ya ngono kazini imeendelea kuwatesa wanawake wengi hususani katika kampuni za watu binafsi, huku wajawazito nao wakiachishwa kazi katika nyakati wanazokwenda likizo ya uzazi.

Hayo yalisemwa na Katibu Msaidizi wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha na Huduma za Ushauri (TUICO), Christina Muchuruza, wakati akizungumza katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika jana katika viwanja vya Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) jijini Dar es Salaam.

Alisema wafanyakazi wengi katika kampuni nyingi binafsi wamekuwa wakiombwa rushwa ya ngono na baadhi yao kupoteza kazi kabisa kutokana na vitendo hivyo.

"Sisi tumekuwa tukikumbana na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi katika kampuni nyingi hasa binafsi, wafanyakazi wa kike wanakumbana na tatizo kubwa la kuombwa rushwa ya ngono na hili limekuwa changamoto kubwa kwetu kwa sababu tunapotaka kuwasaidia wengi huwa wanaogopa kutoa ushirikiano kwa kuhofia vitisho vya kufukuzwa kazi na kudhalilika," alisema Muchuruza.

Aliongeza: "Kwa sababu sisi kazi yetu ni kutetea wafanyakazi, hatutoi siri ya mtu anayetoa taarifa au anapokuja kumshtaki mwajiri wake pale anaponyanyaswa na tumekuwa tukiwaelimisha kila mara kuhusu hili, lakini bado wafanyakazi wengi wanaogopa kuonyesha ushirikiano katika kushughulikia unyanyasaji huu na hata wachache wanaoripoti, tunapofikia hatua ya kwenda mahakamani hawatoi ushahidi na ndiyo maana inakuwa changamoto kulishughulikia."

Kuhusu wanawake wanaokwenda likizo ya uzazi, Muchuruza alisema wengi katika kampuni hayo binafsi wamekuwa wakikosa kazi baada ya kwenda likizo ya uzazi.

"Tumegundua kwamba wanawake wengi wanapokwenda likizo ya uzazi na wanaporudi kazini huwa wanakuta nafasi zao zimechukuliwa, kwa hiyo hili nalo tumeshaanza kulifanyia kazi na limeanza kuzaa matunda," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alisema takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015/2016 zinaonyesha kuwa vitendo vya ukatili wa kingono vinaongezeka kulingana na umri.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kuwa asilimia nane ya wanawake wenye umri kati ya 15 hadi 19 wamekumbwa na ukatili huo.

Liundi alisema ripoti ya idadi ya watu duniani ya mwaka 2019 inaonyesha kuwa asilimia 35 ya wanawake wote duniani wamekutana na aina mbalimbali za ukatili ikiwamo udhalilishaji wa kingono katika maisha yao.

Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Nyanda Shuli, aliwaomba wafanyakazi na wengine wanaofanyiwa ukatili kutoa taarifa ili zifanyiwe kazi na kwamba serikali haitavumilia ukatili wa aina yoyote kuendelea kufanyika.

Alisema serikali imekuwa ikitumia asilimia 3.5 ya pato lake kuhudumia waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

## Agizo kukamilisha madarasa 2,800

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, ameziagiza halmashauri mkoani humo kuhakikisha zinakamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,888 ili wanafunzi waliokosa nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza waweze kwenda sekondari.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akifungua kikao cha kamati ya ushauri mkoa wa Rukwa (RCC) katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema wanafunzi waliofaulu darasa la saba mwaka 2019 ni 16,069, kati ya hao wavulana ni 7,953 na wasichana ni 8,116, na nafasi zilizopo ni 13,128.

Wangabo alisema kuwa wanafunzi ambao watakosa nafasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ni 361, Wilaya ya Nkasi wanafunzi 1554, Wilaya ya Sumbawanga Manispaa ni wanafunzi 179 na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni wanafunzi 794.

Kutokana na takwimu hizo Halmashauri ya Nkasi inaongoza kwa kuwa na wanafunzi wengi watakaokosa nafasi ikifuatiwa na Halmashauri ya Sumbawanga, Kalambo na Halmashauri ya Manispaa.

Aidha, Wangabo aliwaagiza wakuu wa wilaya za mkoa huo kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliofaulu wanajiunga kidato cha kwanza ifikapo Januari 2020, na kuwa hakutakuwa na udahili wa pili wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2020.

Kwa upamde wake, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa (CCM), Silafi Maufi, alishauri kuwapo utaratibu wa kuwapima mimba wanafunzi mara kwa mara kuliko kusubiria mpaka mwanafunzi ahisiwe kuwa na ujauzito, na kwamba wanaume waliosababisha mimba hizo wakamatwe na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Mkoa huo wa Rukwa una jumla ya wanafunzi 294 waliokatisha masomo kutokana na kupata ujauzito katika kipindi cha mwaka 2019.

# Sababu kukithiri rushwa ngono hii

**Na Mary Geofrey**

KUKITHIRI kwa rushwa ya ngono kumetajwa kuchangiwa na utolewaji mdogo wa taarifa kutoka kwa wahusika kutokana na jamii kukosa utayari.

Kutokana na changamoto hiyo, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru), imeanza kufanya utafiti wa kuanza kukusanya taarifa kamili juu ya rushwa ya ngono ili kupata takwimu hizo.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Mfuko wa Uhifadhi Wanawake Tanzania (WFT), Mary Rusimbi, wakati akizungumza juzi jijini Dar es Salaam kwenye kongamano la kujadili masuala ya rushwa ya ngono ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) na kufadhiliwa na Mfuko wa Wanawake nchini (WFT).

Alisema ni vema mapambano juu ya rushwa ya ngono yanahitaji kuongozwa na tafiti ili kujua ni wapi wanaweza kuanzia katika kupambana na rushwa hiyo ambayo ni ukatili. “Hadi sasa kuna asilimia 98 ya unyanyasaji wa kijinsia hivyo ni muhimu jambo hili kushirikisha watu wote hususani ngazi za familia kutoa ushirikiano na kuhakikisha watu wanaofanya vitendo hivyo kuchukuliwa hatua za kisheria,” alisema Rusimbi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Rose Reuben, alisema kulazimisha ngono na kutoa rushwa ya ngono kwa namna yoyote ni kosa la jinai. Alisema jamii inajukumu kubwa la kutoa taarifa na kuhabarishana kwasababu rushwa ya ngono inamadhara makubwa ikiwamo maambukizi ya maradhi ya ugonjwa wa Ukimwi kuongezeka kwa kasi.

“Maadili kwa sasa yamebadilika sana na teknolojia imeongezeka hivyo ni vyema taarifa za rushwa ya ngono na unyanyasaji mwengine wa jinsia ufanyiwe kazi na upingwe kwa kuunganisha nguvu ya pamoja na wadau mbalimbali,” alisema Rose. Naye Mwakilishi kutoka Jeshi la Polisi, Janeth Magomi, alisema jukumu la jeshi hilo ni wasimamizi wa sheria na wamekuwa wakifanya kazi katika shule, vyuoni na maofisini kuhakikisha wanatoa elimu juu ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia.

“Tumekuwa tunapokea kesi nyingi kupitia madawati yetu ya kijinsia kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia unaofanywa na watu na hatua mbalimbali tunazichukua dhidi yao,” alisema na kuongeza.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akikagua magari katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Tofali chanzo kipya mapato halmashauri

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

HALMASHAURI ya mji wa Masasi mkoani Mtwara, imebuni mradi wa ufyatuaji tofali na kuziuza kwa jamii ukiwa ni mpango mkakati wa kubuni vyanzo vya mapato ya ndani ili kujiongezea mapato ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alipokuwa akizungumza na watendaji na madiwani wa halmashauri hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa za maendeleo ya kata kwa robo ya kwanza.

Alisema lengo la halmashauri la kubuni mradi huo ni kuwa na vyanzo vingi vya mapato vitakavyoiongezea halmashauri hiyo mapato ya kutoka na kuweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Ntavyo alisema mradi huo utaongeza thamani ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na kwamba fedha hizo ambazo zitatokana na mradi huo wa uuzaji matofali zitasaidia kutekeleza miradi ya halmashauri. Alisema kwa sasa halmashauri hiyo inafyatua matofali ya inchi sita ambayo yatauzwa kwa Sh.1,600 kwa tofauli moja

Alisema matofali hayo yatauzwa kwa mtu yeyote ambaye anahitaji tofauli kwa ajili ya ujenzi, hivyo kila mmoja anawajibu wa kuifahamisha jamii juu ya uwepo wa mradi huo ili uweze kuleta tija kwa halmashauri. “Katika kubuni vyanzo vya mapato kwa halmashauri yetu tumeona tubuni mradi wa kufyatua matofali ili uweze kutuingizia fedha kupitia mapato ya ndani hii ni fahari kwetu,” alisema Ntavyo.

Aidha, Ntavyo aliwataka watendaji na madiwani kuendelea kuhamasisha jamii kuchangia nguvu kazi katika ujenzi wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao. Alisema kila mmoja kwa nafasi yake lazima atambue na kuchangia katika kufanikisha miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Sospeter Nachunga, alishauri watendaji na madiwani kutathmini na kusimamia vema fedha zinazotolewa na serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

# Waonywa dhana potofu afya uzazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JAMII imetakiwa kuachana na dhana potofu ya kudhania kuwa kuwafundisha watoto kuhusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango ni kuwafanya waanze kujiingiza kwenye uhusiano wa kingono katika umri mdogo.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Anastazia Tutuba, alisema usiri uliopo kwenye jamii husababisha watoto wengi kujiingiza katika vitendo vya ngono katika umri mdogo na kupata mimba za utotoni.

Tutuba aliitaka jamii hususani wazazi kuvunja ukimya na kuweka utaratibu wa kuzungumza na watoto wao kuhusiana na afya ya uzazi wa mpango kwa kuangalia mabadiliko yao ya kimwili na kiakili yanayojitokeza kipindi cha ukuaji.

Alisema serikali na mashirika binafsi vimeweka mipango ya maendeleo kwa jamii na taifa ili kulinda kizazi cha vijana kisiteketee.

"Tuungane kuwafundisha vijana wetu kuhusu afya ya uzazi wa mpango ili kuwa na kizazi kinachojitambua na kutambua majukumu yao binafsi na ya taifa badala ya kuwa na kundi la vijana lililojeruhiwa na uhusiano kitendo kinachowasababishia msongo wa mawazo," alisema Tutuba.

Pia aliwataka walimu wa afya katika shule za msingi na sekondari kuanzisha klabu za afya na kuwafundisha masomo ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango ili kuwajengea uwezo vijana wa kujitambua kimwili, kiakili na kisaikolojia.

Ofisa Vijana wa Halmashauri hiyo, Ahadi Mlay, ukosefu wa elimu kwa jamii kuhusu afya ya uzazi kwa vijana imekuwa tatizo linalokatiza ndoto za vijana kufikia malengo.

Aidha, aliitaka jamii kutoa elimu kwa vijana na kuwashauri kufika katika vituo vya afya vya kutolea huduma kupewa elimu ya afya ya uzazi.

Halmashauri ya Arusha DC, kwa kushirikiana na Shirika la Jhpiego Tanzania inatekeleza mradi wa "Tupange Pamoja Huduma Rafiki kwa Vijana" unaofadhiliwa na Taasisi ya Bill & Melinda Gate ya Marekani.



Daktari wa Mifugo, Deo Temba (kushoto), ambaye ni Mkurugenzi wa kiwanda cha maziwa cha The Grande Demam, akitoa maelezo kuhusu elimu ya dawa za mifugo kwa wananchi waliotembelea banda lake, katika maonyesho ya dawa za mifugo yalioandaliwa na Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA), katika viwanja vya ofisi ya mifugo jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Asisitiza mafunzo ya watumishi kazini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

VYUO vya elimu ya juu na mafunzo ya ufundi vimeshauriwa kuandaa mpango mkakati wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma ili kuwaongezea ujuzi na maarifa.

Mafunzo hayo yameelezwa kuwa yatawawezesha kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoikabili dunia kwa sasa sambamba na kufanikisha azma ya serikali ya kuutumikia umma.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Alvera Ndabagoye, katika wa kufunga mafunzo yaliyotolewa na Chuo cha Uhasibu Arusha, kwa wakuu wa shule na walimu wa fedha.

Mafunzo hayo yalihusiana na saikolojia ya uongozi na usimamizi wa fedha za umma. Ndabagoye alisema mafunzo kazini ni nyenzo muhimu kwa watumishi kwa kuwa huwaongezea tija na ufanisi kazini pamoja na utendaji kazi wao.

Alisema licha ya watumishi kuwa wameajiriwa kutokana na taaluma zao, bado kuna haja ya kupata mafunzo kazini ambayo yatawaongezea weledi na ufanisi zaidi. "Serikali inashindwa kumudu kuwapeleka watumishi kwenye mafunzo, kutokana na gharama kubwa zinazopangwa na vyuo kulingana mafunzo yenyewe," alisema Alvera.

"Unakuta chuo kinaandaa mafunzo kwa ajili ya watumishi wa kada mbalimbali lakini gharama kwa mtu mmoja ni laki mbili na kuendelea na ukiangalia halmashauri yetu ina watumishi 8,000 hivyo ni vigumu kumudu gharama," aliongeza.

Mkuu wa IAA, Prof. Eliamani Sedoyeki, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watumishi wa serikali kusimamia vizuri rasilimali za umma.

Aidha, alisema chuo hicho kimeandaa mpango wa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakuu wa shule na walimu wa fedha ili kusimamia matumizi sahihi ya fedha. "Kumekuwa na tatizo la matumizi mabaya ya fedha kwa shule za serikali pia kutokuwa na wahasibu ambao si wasimamizi wa fedha jambo linalosababisha kusuasua kwa taarifa za utunzaji wa fedha," alisema Sedoyeka.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Oldonyosambu, Richard Migabuso, alisema mafunzo hayo yatawaongezea maarifa ya usimamizi wa fedha za umma hususani kwenye kipengele cha ulinganifu wa hesabu.

# Wataka uchunguzi kifo cha kada wa Chadema

**Na Allan Isack,** MANYARA

MWILI wa aliyekuwa mgombea wa nafasi ya ujumbe kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa katika mtaa wa Mnara wa Voda jijini hapa, Sirili John, ulizikwa jana katika kitongoji cha Lamai, Hanang mkoani Manyara.

Kwa mujibu wa taarifa za awali kutoka Jeshi la Polisi mkoani Arusha, John aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali.

Awali, Jeshi la Polisi mkoani Arusha lilisema bado linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo, lakini wananchi wamelitaka jeshi hilo kuchunguza kifo hicho kutokana na kuhusishwa na masuala ya kisiasa.

Wakizungumza juzi na Nipashe, wakazi wa kitongoji cha Lamai, walidai kuwa polisi wanaposema John alijiua hawaamini kutokana na mazingira ya kifo chake kuwa ya utata.

James Hamis alisema kama ilivyosemekana alijiua kutokana na msongo wa mawazo ni jambo gumu na lisilowezekana na haliwaingii akilini mwao.

"Sirili alikuwa mfanyabiashara wa matunda eneo la Friend's Corner jijini Arusha na alikuwa kada maarufu wa Chadema (Chama cha Demokrasia na Maendeleo)," alisema Hamis.


Alisema walisikia alichukua fomu ya kugombea nafasi ya ujumbe wa serikali ya mtaa wa Mnarani na chama chake hakikujitoa kwenye uchaguzi uliofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Magdalena Albert, mkazi wa eneo hilo, alisema Jeshi la Polisi linapaswa kutoa majibu ya uhakika ili kuondoa sintofahamu iliyopo ya mazingira ya kifo cha John. "Huyu kijana hakuwa na tatizo na mtu na tumeishi naye hapa Lamai na baadaye alikwenda Arusha kutafuta maisha. Tunaomba uchunguzi ufanyike," alisema Albert.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema bado wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo. Pia alikanusha tukio hilo kuhusishwa na masuala ya kisiasa.

Alisema uchunguzi wa awali ulionyesha kwamba John hakugombea nafasi yoyote ya uongozi katika vyama vya siasa.

Aidha, alisema alifika eneo la tukio baada ya kupata taarifa hizo na walikuta chumba kikiwa kimefungwa kwa ndani na funguo zikining'inia kwa ndani ya mlango. "Watupe nafasi ya kuchunguza kwani inadaiwa hivi karibu huyo kijana alitaka kujiua baada ya kuachana na mwanamke aliyekuwa anaishi naye ambaye inasemekana alimwibia fedha," alisema.





# Wataka viungo maiti vitolewe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro, Mawenzi ipo katika mpango mkakati wa kuwaelimisha wananchi waruhusu wanapofiwa na ndugu zao, miili yao iondolewe baadhi ya viungo ili kuwekewa wagonjwa wenye uhitaji wa viungo hivyo.

Hayo yalibainishwa na Mganga mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Japhet Boniface wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilipotembelea hospitali hiyo kukagua ujenzi wa jengo la mama na mtoto ukiwa ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

Dk. Boniface alisema mpango huo utakapoanza, utasaidia wananchi kuepuka kwenda nje ya nchi kuwekewa baadhi ya viungo kama figo kwani zitakuwa zikiwekwa katika hospitali nchini.

"Tunataka kuanzisha mpango maalum wa kuwaelimisha wananchi kuruhusu ndugu zao wanapofariki basi tuweze kutoa baadhi ya viungo kwa ajili ya kuwawekea watu wengine wenye uhitaji wa viungo hivyo, hali itakayosaidia Watanzania kutotumia gharama kubwa kwenda nje ya nchi," alisema Dk. Boniface.

Akizungumzia suala la ujenzi wa jengo hilo la mama na mtoto, Dk. Boniface alisema kuwa jengo hilo la ghorofa tatu linatarajiwa kugharimu serikali kiasi cha Sh. bilioni 12 hadi kukamilika pamoja na vifaa vyake.

Alisema jumla ya Sh. bilioni 4.7 zimeshatumika katika ujenzi wake ambapo fedha hizo ni ruzuku ya serikali, huku pia akidai kuwa hospitali hiyo ambayo ni pekee Kanda ya Kaskazini inayohudumia wagonjwa wa akili, lakini inakabiliwa na uhaba wa daktari bingwa wa magonjwa hayo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alishangazwa na kitendo cha kusimamishwa kwa ujenzi wa jengo hilo, huku fedha za kuendelea na ujenzi huo zikiwa zimeshatolewa na serikali.

"Sisi kama wasimamizi wa ilani hatuaridhishwi kuona fedha za kuendeleza ujenzi huu zimeshatolewa na serikali, lakini ujenzi umesimama hivyo niiombe Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mkandarasi wa ujenzi huu ambao ni Wakala wa Majengo (TBA) kuhakikisha ujenzi huu unaendelea ili kuwanufaisha wananchi," alisema Boisafi.

Alisema kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC kutokana na baadhi ya huduma muhimu za mama na mtoto kutolewa katika hospitali hiyo ya Mawenzi.

Aidha, Boisafi aliutaka uongozi wa hospitali hiyo kubuni michoro ya kujenga majengo yake kwenda juu kutokana na eneo la hospitali hiyo kuwa dogo na kuwataka kuanza na jengo la dharura ambapo serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya jengo hilo.

Kamati hiyo ya siasa Mkoa wa Kilimanjaro pia ilitembelea mradi wa kituo cha mabasi cha kimataifa cha Ngangamfumuni Manispaa ya Moshi ambapo ujenzi wake unaendelea na mpaka kukamilika kwake kitaigharimu serikali Sh. bilioni 28.864.

Kituo hicho ambacho kitakuwa ni cha kwanza kujengwa nchini kina uwezo wa kuhudumia mabasi 72 kwa wakati mmoja, huku abiria zaidi ya 640 wakihudumiwa kwa wakati mmoja.

Mpaka sasa serikali imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni 8.766 katika ujenzi wa kituo hicho, ambapo mwenyekiti huyo aliwataka makandarasi kufanya kazi kwa uaminifu mkubwa kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha pamoja na kulinda mali zilizopo katika eneo hilo.



Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kisangara wilayani Mwanga, Dk. Regina Kilangali, akionyesha baadhi ya vifaa tiba vilivyotolewa na serikali, baada ya kukamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji, maabara na wodi ya wazazi, kituoni hapo, juzi. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# RC amjia juu ofisa wa manunuzi

**Na Mary Mosha,** SIHA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amemtaka ofisa manunuzi wa Halmashauri ya Siha, Costantine Nkya, kuandika taarifa ya upungufu wa usimamizi mbovu katika majengo ya hospitali ya wilaya hiyo.

Akizungumza kwenye kikao cha watumishi wa halmashauri sambamba na kumtambulisha katibu tawala wa mkoa huo, Abibu Kazungu.

Alisema awali majengo hayo ya hospitali yangekamilishwa kwa Sh. 1.5 bilioni, lakini kutokana na usimamizi mbovu inadaiwa zinahitajika tena nyongeza ya kiasi cha Sh. 370 milioni kumalizia ujenzi huo.

"Hapa ofisa manunuzi umeshindwa, mhandisi umeshindwa, kamati imeshindwa... hatuko salama sana, hii hospitali naomba taarifa yako niipate haraka nijue chakufanya," alisema Mghwira.

Mghwira alisema kuwa hospitali hiyo ilitakiwa kukamilisha ujenzi wake mapema mwezi Julai mwaka huu, lakini sasa mwaka unaelekea kumalizika milango na vitasa havijulikani vilipo.

"Nitachukua hatua moja hadi nyingine kuhakikisha hospitali inasimama, na hizi fedha kiasi cha shilingi milioni 370 zinazotakiwa kumalizia ujenzi hazijulikani zitapatikana kwa njia ipi kutokana na uzembe uliojitokeza," alisema zaidi Mghwira.

Alisema kitendo cha milango kutengenezewa Dar es Salaam kimechukua muda mrefu kufika kwake licha ya majengo kukamilika jambo ambalo linakwamisha jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya afya.

# Viongozi wapya watakiwa kuwa chachu ya maendeleo

**Na Mary Mosha,** KILIMANJARO

WENYEVITI wa vijiji na vitongoji waliochaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika mwezi huu katika Halmashauri ya Moshi, wametakiwa kuwa chachu ya maendeleo katika nafasi zao badala ya kuwa kikwazo.

Akizungumza baada ya hafla ya kuwaapisha viongozi hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Castor Masijara, alisema wenyeviti hao wanao wajibu wa kuhakikisha miradi ya kimaendeleo inayotekelezwa na serikali inafanyika kwa ukamilifu.

Alisema serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya kimaendeleo katika maeneo mbalimbali, lakini wamekuwapo baadhi ya wenyeviti wa vijiji ambao huleta ukiritimba, hivyo kukwamisha miradi hiyo kutekelezeka kwa wakati.

"Mwende mkawe daraja kuwaunganisha wananchi na serikali ili miradi ya kimaendeleo iweze kukamilika kwa wakati badala ya miungu katika maeneo mnayoongoza kwa hali hiyo hatutaweza kupiga hatua," alisema Castor.

Katika hatua nyingine, aliwataka kutokuwa chanzo cha migogoro katika jamii na badala yake wawahudumie wananchi kama ilivyo dhamira ya serikali katika kutatua kero za wananchi.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Moshi, Juma Tukosa, alisema muda wa siasa umemalizika na viongozi halali wamepatikana kwa mujibu wa sheria.

Alisema wapo baadhi ya wanasiasa ambao hawataki kuamini kuwa wananchi wametumia haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka badala yake wanataka kuleta malumbano ambayo hayana tija kwani muda huo haupo.

"Nyie mmepewa dhamana na wananchi, hivyo msije mkayumbishwa na mwanasiasa yeyote muda wa malumbano na siasa zisizo na mashiko haupo, kilichobaki ni nyie kuchapa kazi kwa wale waliowachagua kwa sababu waliwaamini," alisema Tukosa.



Ukurasa 18

Profesa Stiglitz: Uliberali huria umekwisha, historia mpya sasa



Ukurasa 14

DC Busega 'anyunyiza' simulizi ya wanavyokwea kupitia 'hapa kazi'


# BUFE

Ijumaa Novemba 29, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 20

## Mbunge Maige adokeza wapi Veta inasimamia pengo ajira



# Handeni inapogeuza maajabu na utajiri wake kuvutia watalii

**Na Christina Haule,** HANDENI

AWALI dhana ya utalii iliishia katika maeneo ya uhifadhi na wanyama. Lakini, hivi sasa imepanuka zaidi, ikiwamo maeneo mengi, mbali na ya kihistoria za siku nyingi kama vile Bagamayo.

Katika mabadiliko hayo ya kupanua wigo, serikali wilayani Handeni, jijini Tanga, inakusudia kuboresha na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo, ikiwamo msitu wa Talawe uliopo kwenye Tarafa na kijiji cha Mazingara.

Hapo ni mahali penye msitu mnene na mapango makubwa yenye nyoka, kungwi na mwali na malikale (vifaa), zilizoachwa na Mwalimu Julius Nyerere.

Ufafanuzi huo unatoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni jijini humo, Mwalimu Boniface Juma anayeeleza hayo, katika ziara ya mafunzo ya wanahabari kwenye msitu huo, kupitia Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC).

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Kinamama Mafia 'hawajambo' kibiashara, tishio kuu usafiri

Ukurasa 19

BIASHARA

# DC Busega 'anyunyiza' simu wanavyokwea kupitia 'hapa

• Aibua ombi 'utumbuaji' ufike chini yao



Hospitali ya Wilaya Busega. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Anthony Gervas,** BUSEGA

BUSEGA ni miongoni mwa wilaya tano zinazounda Mkoa wa Simiyu. Zingine ni Bariadi, Meatu, Maswa na Itirima. Kabla, ilikuwa jimbo la uchaguzi la Busega Vijijini, katika Wilaya ya Magu, Mkoa wa Mwanza.

Wilaya hiyo ilianzishwa mwaka 2012,katika kipindi ilipoanzishwa mikoa mipya mbalimbali nchini. Katika uhai wake mpya, sasa inajigamba kuwa katika serikali ya awamu ya tano ya Rais, Dk. John Magufuli, ikipiga hatua kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ya wananchi kwa mafanikio.

Kihistoria, ni wilaya pekee kutoka mkoa Mwanza, kuunda Simiyu, zilizobaki zinatoka mkoa Shinyanga.

Hadi sasa Busega, kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2012, ina wakazi 203,597 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 2,129, asilimia 28 ikiwa ni maji sehemu kubwa ni Ziwa Victoria na inapakana na Mkoa wa Mwanza, ikiwamo kisiwa Ukerewe na wilaya Serengeti, mkoa Mara.

**ORODHA MAENDELEO**

Shughuli kuuza kiuchumi kwa wananchi hao ni kilimo, ufugaji, uvuvi pamoja na biashara, huku Mkuu wa Wilaya, Tano Mwera, anasema kuna ushuhuda wa kasi ya maendeleo na uchumi kutokana na kasi ya miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi, kwenye maeneo kama afya, elimu, kilimo, maji na uboreshaji miundombinu ya barabara.

Mkuu wa Wilaya ya Busega Mwera, alipozungumza na Nipashe ofisini kwake wiki hii, anataja miradi ya ufugaji samaki aina ya sato kupitia mabwawa maalumu, kwa ajili ya kuongeza tija katika wilaya

> **"Wakati mimi nikiteuliwa na kuwa Mkuu wa Wilaya ya Busega mwaka 2016, maendeleo ya wananchi yalikuwa chini sana kuliko sasa hivi.**




Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (wa pili kushoto), akitoa maelekezo kwa mhandisi mshauri alipoutembelea Mradi wa Maji Lamadi, wilayani Busega.

"Wakati mimi nikiteuliwa na kuwa Mkuu wa Wilaya ya Busega mwaka 2016, maendeleo ya wananchi yalikuwa chini sana kuliko sasa hivi," anafafanua na kuendelea: "Masuala ya uwajibikaji yanatekelezwa katika sekta zote za umma, wananchi wanahudumiwa bila kuzungushwa."

Mwera anasema, katika utekelezaji sera za maendeleo ya wananchi, huduma bora sasa zinatolewa katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, kilimo, maji, ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mkuu wa Wilaya anaanza na sekta ya afya, kwamba kuna miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa na kwa sasa kuna ujenzi wa hospitali ya wilaya iliyofikia hatua za mwisho kukamilika, ikigharimu kiasi cha Sh.bilioni 1.5.

Anasema, wanachokisubiri sasa ni kuongezewa fedha na serikali kuu, kiasi cha Sh.milioni 500 kinachohitajika kwa ajili ya kukamilishia vifaa vya kutoa huduma na kwamba, hospitali hiyo inatarajiwa kuanza kutoa huduma rasmi mwaka ujao.



Mkuu

# lizi ya a kazi'







wa Wilaya Busega, Tano Mwera.

Pia anaunganisha hoja hiyo na kuboresha vituo vya afya viwili vya Igalukilo na Nassa, vinavyotoa huduma za upasuaji wagonjwa, huku kukikarabatiwa Kituo cha Afya Lukungu ambacho baadaye kitaanza kutoa huduma za upasuaji na kuna Kituo cha Afya Kiloleli anachosema kinaboreshwa.

Mwera anasema, walipata ufadhili kutoka wa Mradi wa Lipa kwa Ufanisi (BRF), kwa ajili ya kusaidia ukarabati wa zahanati na vituo vya afya, ambavyo kila moja kilipewa fedha Sh. milioni 10.

Anaoanisha hilo na bajeti yao ya upatikanaji dawa katika zahanati na vituo vya afya kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD), anayoitetea kwamba inaridhisha na haina malalamiko, kama ilivyowahi kuwapo awali.

Katika kufanikisha hilo, mkuu wa wilaya anawahamasisha wananchi kujiunga na Bima ya Afya iliyoboreshwa (CHF), ili kinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, wapate huduma ya matibabu bure.

"Dawa muhimu zote zinapatikana kwa wagonjwa,sisi wilaya yetu hatuna shaka na hilo," anasema.

**HUDUMA MAJI**

Mkuu wa Wilaya anasema utekelezaji wa miradi ya maji katika Kata ya Kiloleli, umekamilika na utagharimu kiasi cha Sh.bilioni 1.6 mradi wa Kata ya Nyashimo katika makao makuu ya wilaya hiyo nao unaendelea kutekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.8.

"Upo mradi mkubwa zaidi wa maji unaojengwa katika kata ya Lamadi, ambao utahudumia kata nzima na vijiji vingine vya jirani, utakaogharimu kiasi cha Sh. bilioni 12 unaofanyiwa majaribio sasa. Unakisiwa kuhudumia zaidi ya kaya 33,000 ifikapo mwaka 2030, kadri watu wanavyozidi kuongezeka," anasema Mkuu wa Wilaya Mwera.

**ELIMU IMEKAAJE?**

Katika elimu, Mwera anaanza na taarifa ya kiwango cha ufaulu kilichoongezeka mwaka jana, kufika zaidi ya asilimia 70 na mwaka huu 2019 imekwea zaidi hadi asilimia 90 ya wanafuzi wote wa shule za msingi, kukiwapo wanafunzi wanne walioingia katika kundi la 'kumi bora' za wanafunzi kujiunga sekondari kutoka shule za msingi.

Anasema kupanda kiwango cha ufaulu huo, umeleta chachu kwa watoto kuandikishwa shule za msingi, kutokana na sera iliyopo ya' elimu bure' ambayo katika sura ya pili, inachangia ongezeko kubwa la wanafunzi shuleni na kuangukia shida ya upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya anasema, malengo yao katika wilaya mwaka uliopo wa fedha ni kujenga zaidi shule za sekondari kila kata, kutoka moja hadi shule tatu, ili kuondoa changamoto za wanafunzi wanaofaulu darasa la saba kuingia sekondari wasikose nafasi, katika wilaya hiyo yenye kata 15.

Mkuu huyo wa Wilaya, anasema mwaka juzi walijenga shule za sekondari tatu, anazozitaja kuwa: John Mtaka, Dk. Chegeni na Masanza Kona na mwaka jana zilijengwa sekondari mpya mbili ambazo ni Nyamikoma na Gininiga.

**MIRADI BARABARA**

Anaeleza kuwa, barabara ndani ya wilaya hiyo zimejengwa na kuunganisha kata moja na nyingine, chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (Tarura).

"Makandarasi waliokuwa 'makanjanja' katika halmashauri za wilaya sasa hawapo tena, baada ya serikali kubadilisha mfumo wa usimamizi wa barabara hizo na kuwapa Tarura. Ndiyo maana, barabara zinajengwa kwa kiwango kinachotakiwa na haraka.

"Mikataba ya ujenzi inasimamiwa na mkoa na kupewa tenda makandarasi wenye sifa. Sio mtu anabeba begi tu na makaratasi anapewa tenda ya kujenga barabara, hana hata vifaa vya ujenzi. Hivi sasa mpaka awe na vigezo," anasema Mwera.

Anafafanua kwamba kabla ya Tarura kupewa usimamizi, kuna wanasiasa na watendaji waliochukua tenda za ujenzi kwa maslahi yao binafsi, jambo lililoleta mvutano na changamoto nyingi katika kuwafikishia huduma muhimu wananchi wake.

Mkuu wa Wilaya anasema, pia sasa wanaendelea kupambana na uvuvi haramu wa kutumia zana zilizozuiliwa na serikali kutumika kuvulia samaki wadogo, hivyo wanawachukulia hatua za kisheria.

Mkuu huyo wa wilaya, anajigamba kuwa miradi yote inasimamiwa vyema sasa pasipo ubadhirifu na anatumia uthibitisho wa mwenge wa uhuru ulipozuru hapo mwaka huu, wakimbizaji walikagua miradi hiyo na hapakuwapo miradi chini ya viwango na kukataliwa.

Mwera anahitimisha kwa kumpongeza Rais Dk, Magufuli na kutoa rai ya kuwapo watendaji wa ngazi za chini yao wakuu wa wilaya, akiwatuhumu wanakwamisha shughuli zingine za maendeleo.

Anafafanua, bila ya kutaja vyeo vya wanaotuhumiwa, akisema: "... watendaji wanaotukwamisha sisi wa juu na kusababisha sisi tunafanya kazi kwa 'presha' kubwa, nao tunaomba wawajibishwe kwa haraka, kama ilivyo kwetu"

*• **Mwandishi wa makala hii anapatikana Kanda Ziwa, kwa barua pepe; anthonygervas@yahoo.com, Simu (+255) 0682 86 92 44.***

# Mageuzi ATM za kuuza maziwa



Ndivyo ilivyo ATM ya kuuza maziwa. **PICHA: BBC**



WENGI wanaposikia msamiati 'ATM' kitu cha kwanza wanachowaza ni chombo cha kutolea fedha benki.

Jambo ambalo ni tofauti huko kinatokea mkoani Kilimanjaro ipo 'ATM' ya kwanza ya maziwa, ambayo imegeuka kivutio kwa wakazi wengi katika mauzo ya maziwa.

Unaweza ukajiuliza 'ATM; hiyo inafanyaje kazi? Nancy Manase ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa maziwa anafafanua: "Uone labda tulikuwa tunauza lita mia tatu kwa siku au mia nne, sasa tumeongezea lita mia moja juu.

" Kwa hiyo, ni faida na msimu huu ni ule msimu unaokuwa na maziwa mengi sana, huku kwetu maziwa yanakuwa mengi mpaka yanamwagwa, kwahiyo mpaka sasa hivi hatujamwaga maziwa".

"ATM inatusaidia na watu wamepata elimu kunywa maziwa, ni afya kwa sababu hata usipokula kitu kingine inakutosha," anasema.

Kila lita moja inagharimu wastani wa dola moja (Sh. 2,300), lakini katika mashine hii unaweza kununua maziwa ya kiwango chochote kulingana na hela ulionayo

"Kwa muda mfupi niliyokuwa hapa katika 'ATM' hii ya maziwa mkoani Kilimanjaro changamoto kubwa inayoukabili mradi huu uliotokea kupendwa na walio wengi ni nishati ya umeme, iwapo umeme utakatika basi ni vigumu kupata huduma"

Wafugaji mmoja baada ya mwingine huleta maziwa yao hapa kwa ajili ya vipimo na kuandaliwa tayari kwenda kwenye 'ATM' na kwa upande wa wafugaji, wanasema wameanza kuyaona matunda ya uwapo wake.

Aleningwasa Swai ni mfugaji ambaye ananufaika na huduma hiyo anayesema: "Maziwa yalikuwa hayana bei yalikuwa yananunuliwa 'kirojorojo' tu.

"Lakini, tangu huu mradi ulipoanza wa kupeleka maziwa mjini tumepata faida sana, maziwa yanachukuliwa mwisho wa mwezi unakwenda kuchukua hela yako".

Kwa wateja wa maziwa kwenye 'ATM' nao walikuwa na maoni yao kuhusu mradi huo, Martin Karata akisema: "Maziwa ni mazuri nimeshakunywa maziwa sehemu nyingi, maziwa ya hapa nimeona kuna tofauti kidogo.

"Cha kwanza, maziwa yatoka kwenye ATM halafu istoshe maziwa ni mazuri kwa hiyo muda wote mtu ukihitaji maziwa ya kuchemsha na chai unapata muda wowote.", anaeleza mteja wa maziwa."

"Huduma hii ni nzuri ukija kwa muda wowote unapata maziwa, ikiwa asubuhi mchana jioni unapata maziwa," Neema Munisi anasema.

Kwa sasa zipo ATM mbili tu mkoa mzima wa Kilimanjaro na wafugaji wengi wanatamani ziongezwe na kusambaa katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu, kama vituo vya mabasi, hospitalini na sokoni. **BBC**

UCHUMI

# Handeni inapogeuza maajabu na utajiri wake kuvutia watalii

## • Pango walikopotea Mwali, Kungwi • Iliko Kibanga aliyempiga mkoloni •Nyoka adimu abadilishae hali ya hewa

INATOKA UK.13

Juma anasema, kupitia vipaumbele vyao kiwilaya ikiwamo elimu ya kulinda maliasili, kwa kushirikiana na wanavijiji wanaojitahidi kuifanya jamii kuelewa sheria mpya ya maliasili nchini, inayomtaka kila Mtanzania kutambua maliasili inayomzunguka inamhusu.

Anarejea historia, Mwalimu Nyerere alifika eneo hilo na kuacha vifaa mbalimbali alivyotumia na viongozi wengine, ambavyo sasa vinakusanywa katika sehemu moja, kwa ajili ya kumbukumbu na utalii.

Katibu Tawala anasema, pia eneo linaloitwa 'Kwa Chaga' alikotoka mtu aliyefanya tukio la kumpiga mkoloni enzi hizo za ukoloni alijulikana kama 'Kibanga' aliyekataa manyanyaso ya wakoloni na kuamua kumpiga, aliandikwa kwenye vitabu na vinasomwa kwenye shule mbalimbali nchini hivi sasa.

Ni mtazamo mpana anaosema unahusu Tarafa ya Mazingira ambalo wataangalia na kuhifadhi mipaka yake, isiingiliwe kwa ajili ya kuiacha ibaki eneo la utalii wa kihistoria.

Mwalimu Juma anasema, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia programu yake itwayo FORVAC, watafuatilia malengo ya mpango huo yanatimia.

Katika hilo, kuna suala la elimu ya kuboresha bidhaa mbadala kwenye mazao ya misitu waliyoitoa kwa wasimamizi wa misitu na wao watayatangaza maeneo yanayoonekana kuwa vivutio zaidi.

Anasema, wanajipanga kuanza kutengeneza maelezo maalum ya kuijulisha jamii kuwapo vivutio hivyo, sambamba na kutengeneza miundombinu rafiki ya kufika maeneo hayo, kujionea utalii na vituo vya kihistoria vilivyopo na kutangaza utalii huo ndani na nje ya nchi.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni, Mwalimu Boniphace Juma, alipozungumza kuhusu mikakati yao, kulinda rasilimali misitu kwa kushirikiana na Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (Forvac. **PICHA: BLOGU FULL SHANGWE.**

### UCHOMAJI MISITU

Anasema, Handeni ilikuwa na tatizo la watu kuchoma mkaa na kusafisha mashamba, kwa kuchoma moto misitu na kuharibu mazingira kulikotokana na ukosefu wa elimu ya misitu na kwamba FORVAC wamekuja na mbinu mbadala.

Katibu Tawala anaitaja nyingine ya kutoa elimu ya kuboresha mnyororo wa thamani, ikiwamo kuweka mizinga ya nyuki na kusaidia biashara kwa wananchi wapate kipato na kuepuka kuharibu mazingira kwa ajili ya kipato.

Juma anasema, elimu iliyotolewa na program ya FORVAC itasaidia kumfanya mkulima kuboresha mnyororo wa thamani badala ya kuchoma mkaa kwa ajili ya kupata Sh. 35,000 ya gunia moja, jambo linalowafanya kushusha thamani ya msitu wenyewe.

> **"Ni nyoka wanaoonekana kwa nadra na wakati mwingine wanapopita hata jua la mchana, hufifia kuwa mithili ya jioni au asubuhi na wakati mwingine hupita upepo mkali.**

Anataja umuhimu wa kukata, kuchoma mkaa na kutoa magome kitaalamu, kwa kuongeza thamani ambavyo vyote mtu anaviuza na kumuingizia kipato.

Hadi sasa wilaya Handeni ina misitu kwenye vijiji mbalimbali, ikiwamo Mazingara yenye ukubwa wa hekta 1,385.7 kwenye kijiji cha Talawe; Msitu Kitumbi wenye ukubwa hekta 7,827.5, Gole hekta 207.3 na Kwedikabu wenye hekta 5626.

### OFISA MISITU

ofisa Misitu Mwandamizi kutoka Wizara ya maliasili na Utalii, Emmanuel Msofe, anazishauri halmashauri kupitia mpango wa Forvac, kutengeneza Mpango wa Utalii kwenye eneo la Mlima Mazingara, lililopo kijiji cha Talawe, katika Tarafa ya Mazingara wilayani humo, ili kuunda kivutio cha utalii kitakachowaingizia wanakijiji kipato.

Msofe ambaye pia ni Mratibu Kitaifa wa Programu ya Forvac, anasema, simulizi za; binti na mama yake kupotelea kwenye pango' (kungwi na mwali); jiwe la pula mbili na mazoka au majoka, ni vivutio vya utalii kiikolojia, vinavyopaswa kusimamiwa kwa usahihi.

Anasema, wananchi hao wakitengenezewa mpango wa utalii, utawasaidia kipato na maendeleo mengine mengi yanayotokana na mnyororo wa utalii.



Baadhi ya watalii wakifurahia ngoma ya kabila wasambaa, iliyokuwa ikiwatumbuiza usiku. **PICHA: WIZARA YA MALIASILI NA UTALII.**

### MAAJABU YA KITALII

Msofe anabainbisha hafichwi na furaha ya kuona msitu wa asili kutoharibiwa, akitaka ushuhuda wa utunzaji bora wa msitu wilayani humo, unahitaji kuigwa katika misitu mingine.

Msofe anaitaja Handeni ni moja ya halmashauri 10 zinazotekeleza program ya kuendeleza mnyororo wa thamani wa misitu Forvac, akiwahimiza maofisa misitu na wananchi kupitia kamati za kuhifadhi misitu za vijiji, wanaendelea kushirikiana kuitunza.

Kuhusu eneo la utalii loywalo liitwalo Mazoka au Majoka, Mjumbe wa Kamati ya Misitu ya Mazingara wa Talawe, Salehe Mtenguzi, ana simulisi kwamba maeneo hayo yana nyoka wa ajabu, ambao si rahisi kuona ama vichwa wala mikia yao.

Anasema ni nyoka wanaoonekana kwa nadra na wakati mwingine yanapopita hata jua la mchana, hufifia kuwa mithili ya jioni ya asubuhi na wakati mwingine hupita upepo mkali.

Kwa mujibu Salehe, kuna wakati nyoka hao wanapita katikati barabara ya lami, magari husubiri muda mrefu na kuna wakati kuchukua wastani wa robo saa. Milima wanakoishi wameipa jina Mazoka.

"Pia, kuna jiwe kubwa ambalo lina sehemu iliyo kama mfano wa pua ya binadamu, ambalo nalo linafaa kuwa utalii wa kutosha, licha ya kwamba kwa sasa kwa kipindi cha mvua kufika kwake ni tabu, mlima unateleza," anasema.

Ombi lake kwa serikali ni kwamba, iwasaidie kupata uhifadhi wa kitalii, ili iweze kupata watalii watakaokenda kuona utalii uliopo na kuwaingizia kipato kitakachowasaidia kuboresha na kuzidisha uhifadhi na utalii.

### ACHIMBA MIKASA

Diwani Zawadi Bendera, anasema historia anayokiri naye ameikuta, kwamba mahali panapoitwa 'Kungwi na Mwali' desturi yake wakazi wa Pwani tangu miaka iliyopita mwali alipelekwa pangoni kuogeshwa 'kuondoa jasho baya' na kuna historia anayeogeshwa na aliyemuogesha walipotea.

Anaendelea kwamba, iliwafanya waliokuwa wanawasubiri kungwi na mwali watoke kuoga ili wakaendelee na sherehe zingine, walilazimika kukimbia na baadae wakaogopa kabisa kuendelea na tendo hilo pangoni. Hivyo, kwa kutekeleza mila wanabaki kuwaogeshea nyumbani mpaka sasa.

Diwani huyo anasema, kwenye pango hilo kumebaki historia, huku wanakijiji wakiendelea kuchota maji ya matumizi ya kila siku majumbani, maji ambayo hayakauki wala kupungua kutokana na uhifadhi mzuri wa misitu.

Inatajwa kuwa kazi nzuri ya wasimamizi wa Kamati ya Msitu wa Kijiji, inayoundwa na wajumbe 15 waliopewa elimu hiyo na program kupitia mpango wa Forvac.

Hiyo ni programu yenu mtazamo kupitia halmashauri 10 nchini inayohusika nazo, katika mtazamo wa ongeza faida za msitu kiuchumi, kijamii na kimazingira, ikizingatiwa misitu kuwa ni sekta inayobeba mengi yanayopaswa kufuatiliwa na kulindwa kwa karibu.

Programu hiyo iliyoanza mwaka 2018 na inatarajiwa kumalizika mwaka 2022 ina halmashauri 10 zinazotekeleza program hiyo, zimetengwa katika Kongani tatu. Kwanza, ni mkoani Tanga katika halmashauri za Kilindi na Handeni, pia majirani zao Mpwapwa mkoani Dodoma.

Nyingine ni kongano ya Lindi, katika halmashauri za Liwale, Nachingwea na Ruangwa; huku Ruvuma kuna Songea, Namtumbo, Mbinga na Nyasa.



Mjumbe wa Kamati ya Maliasili Tarafa ya Mazingara, wilayani Handeni, Shabani Mtenguzi, alipofafanua kuhusu uhifadhi misitu wanaofanya kijijini kwao.

# Biashara katika picha



Mchuuzi wa machungwa akiwa amepanga biashara yake kando ya barabara, eneo la Chalinze, mkoani Pwani hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA.**



Mchuuzi wa ndizi akikatiza kwenye kivuko cha waenda kwa miguu, wakati akisaka wateja katika eneo la Mianzini, jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: WOINDE SHIZZA**,



Mchuuzi wa kashata akisubiri wateja huku akiwa hajazifunika katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI

PHD 1972 YENYE NOBELI...

# Profesa Stiglitz: Uliberali huria umekwisha, historia mpya sasa

**Na Miki Tasseni**



Profesa Joseph Stiglitz. **PICHA: MTANDAO**

UKINZANI wa kiuchumi ulioinuliwa na Marekani dhidi ya China, wakati kwa jadi Marekani ndiyo mlinzi wa soko huria la kimataifa na China inaonekana kuwa na mfumo wa kulinda 'tunu' za kitaifa zisiingizwe kwenye soko.

Sasa imeleta mkangayiko wa fikra kuhusu uchumi wa dunia. Waliokuwa wanatetea soko huria katika medani ya kimataifa, wanapata tabu kueleza kinachotokea sasa na wanaopinga soko huria kwa kiasi kikubwa, wanachekelea.

Mmoja wa vinara katika mjadala huo, ni Profesa Joseph Stiglitz, aliyeshinda Nishani ya Nobel katika fani ya uchumi, baadaye akawa Mchumi Mkuu wa Benki ya Dunia.

Profesa Stiglitz, aliandika tungo ya udaktari wa falsafa katika uchumi mwaka 1972, akiangalia jinsi soko linavyofanya kazi siyo kwa yale mlaji au mteja anaonyeshwa, ila kutumia vianzio vingine vya yale asiyoyaona, yamejificha.

Ni mwelekeo wa fikra ambao kisayansi unaendana na hisia au dhana ya 'ying' na 'yang,' ambayo ni kama hasi na chanya, kuwa kinachotiririka ni chanya,lakini kinawezeshwa na hasi.

Unaweza kuwaza nini 'chanya' na 'nini' hasi.Katika mazingira ya kawaida, iwe ni maisha ya kifamilia au uuzaji bidhaa.

Unaweza kusema katika suala hili, kuna chanya na hasi ya uchumi wa dunia, pia chanya na hasi ya fikra ya uchumi, ambalo ni eneo pendwa la Profesa Stiglitz.

Katika uchumi wa dunia, chanya ni kukua kwa kasi kwa uchumi wa dunia pamoja na kuwapo misuguano ya kina kuhusu umiliki wa rasilimali na uvunaji (siyo mgawo), kwani hakuna kugawana, kila mtu anavuna kivyake, iwe ni faida au mshahara, kukosa kazi au kujaza pesa benki zisizotumika.

Hasi ni ugomvi ndani ya nchi na kati ya mataifa na maeneo yote mawili yanachangia katika chanya na hasi ya ngazi ya fikra kuhusu uchumi, kama kuanguka kwa himaya za itikadi za kijamaa ni mwisho wa yote.

### VITABU VYAKE

Katika insha ya hivi karibuni ya kutambulisha na kuelezea yaliyomo katika vitabu vyake viwili vya miaka ya karibuni, msomi huyo na mwanaharakati anaiparamia kwa mara nyingine tena dhana au nadharia iliyoenezwa mwaka 1990 na Profesa Francis Fukuyama.

Ilikuwa ni miezi kadhaa baada ya kuangushwa ukuta wa Berlin, Ujerumani, mwezi Novemba 1989. Hivi karibuni, Ujerumani iligubikwa na sherehe za miaka 30 ya tukio hilo la aina yake, Profesa Stiglitz akasema ndiyo 'mwisho wa historia' kwa maana hakuna tena mabadiliko ya msingi katika uchumi na jamii duniani.

> **Dhana ya Profesa Fukuyama bado ni sahihi na hakuna 'historia' mpya tangu 1989 ambayo 'haifiti'ndani ya kilichozungumzwa wakati ule.**

Ni kusema kuwa sasa tumefikia soko huria ndiyo kila kitu na wote tutafaidika.

Siyo vigumu kuhisi, siyo kila msomi au kila mchumi aliyekubaliana na hisia hiyo, lakini kudhihirisha katika ngazi ya kimataifa kuwa siyo sahihi ni jambo lingine.

Halafu ukaja mkasa wa uchumi uliogubika sekta ya kibenki nchini Marekani na soko la hisa kwa jumla mwaka 2007- 2008 na kuathiri uchumi wa dunia kwa undani. Ilikuwa pigo la kinadharia kwa itikadi ya soko huria.

Kimantiki, unaweza kusema kuwa mchango wa hivi karibuni wa Profesa Stiglitz ni kuangalia nadharia alizoinua baada ya mwaka 1990 na hasa dhidi ya Profesa Fukuyama, kuangalia ni jinsi gani mkasa ulioikumba dunia kiuchumi miaka 11 iliyopita, na kilichotokea tangu wakati huo, kinadhihirisha nini katika mjadala huo.

Suala hapa ni kuhamia kifikra au kihisia kama kilichotokea 2008 'kinarudisha historia' au ni sehemu ya kile alichosema Profesa Fukuyama, kwa uchumi wa kiliberali utakuwa na mivutano ya uwekezaji na faida.

Pia, anataja 'mara moja moja'kuna mporomoko wa kina katika sekta moja au nyingine, kama kiwango cha uwekezaji ni kikubwa mno na soko limesinyaa. Ila kinachotokeza baada ya hapo si mageuzi, ni utandawazi bora zaidi.

Tatizo linakuja katika kudhihirisha kuwa nadharia hiyo ni sahihi miaka 11 baadaye, kwani mzozo wa Marekani na China katika biashara unafikia hatua ya kuhoji misingi yenyewe ya 'soko huru' na siyo matokeo hasi katika sekta moja au nyingine katika soko la fedha, hisa au mitaji.

Ina maana kuwa, mfumo wa uliberalii utandawazi umewekwa shakani na wakereketwa wa uchumi wa kitaifa wakiongozwa na |Marekani na wanapata nguvu kote barani Ulaya. Wanajiita majina tofauti, lakini wanaunganishwa na 'uzungu' uliokolea na kumpenda Adolf Hitler.'

### MCHANGO MPYA

Profesa Stiglitz anatoa mchango mpya hivi karibuni, akipanua mantikii ya kitabu chake, 'Globalization and Its Discontents' kwa kuongeza neno 'revisited,' yaani kuangalia upya mada hiyo ya utandawazi na wakinzani wake.

Halafu kuna kitabu cha kawaida zaidi cha 'People, Power and Profits' (Watu wa Kawaida na Nguvu za Wenye Fedha, Dola na Utetezi wa mfumo wa Kuzalisha Faida, tofauti na kujali maisha ya watu.

Suala hapa ni kama anachosema kuhusu vitabu hivyo vinadhihirisha mada ya 'kuzaliwa upya kwa historia,' yaani kuna 'kesho' baada ya ubepari na soko hurua, swali ambalo siyo rahisi kulijibu, hapajawa na ujamaa mpya dhahiri tangu 1989.

Ili kutoa mada yenye uhakika zaidi wa kinadharia, ingebidi Profesa Stiglitz, aache medani hiyo ya uanaharakati ya ndoto ya kuubadili mfumo wa kibepari duniani, yaani utandawazi na soko huria, aiingize migongano hiyo katika dhana ya jumla ya utandawazi.

Kwa mfano, kuna mtazamo anachokitaka Rais |Donald Trump wa Marekani, siyo kuondoa mfumo wa soko huria, ila China ikubali watu wengine waingie katika soko lake kama wao wanavyotaka kuingia kwingine. Pia wabadili mfumo wa siasa ili China iwe nchi ya kawaida isiyo tishio la kiusalama kutokana na mfumo wake.

Ukiangalia kwa karibu, unakuta ndiyo mgogoro kati ya Marekani na Iran, hata kufikia vikwazo vya uchumi ambavyo havijahatarisha mfumo wenyewe nchini Iran lakini vimepunguza ushawishi wake kimataifa.

Mabadiliko yanaendelea katika nchi ambazo bado hazijafikia soko hurua na demokrasia, kwani dola inapokuwa si ya kidemokrasia inachukua sehemu kubwa ya pato la taifa kujihami, inabana uhuru wa kuwasiliana. Uchumi ukikabwa, watu wanadai uhuru.

Kwa maana hiyo, dhana ya Profesa Fukuyama bado ni sahihi na hakuna 'historia' mpya tangu 1989 ambayo 'haifiti'ndani ya kilichozungumzwa wakati ule.

Profesa Stiglitz anaongeza chumvi kusema kuwa utandawazi ulionekana kufuta mikasa ya uchumi kwa wafanyakazi nchi za Magharibi kukubali mishahara midogo, na sasa wamekataa.

Kutaka mishahara zaidi hakubadili mfumo, ila labda msomi huyo angetaka kusema wako tayari kuwa na serikali za kimapinduzi.

BIASHARA

# Kinamama Mafia 'hawajambo' kibiashara, tishio kuu usafiri

- Wafunzwa bidhaa kibao za nazi zao
- Hakuna usafiri wa Dar unaoaminika
- Siku 3 wasubiria wataondokaje Rufiji
- Familia ya mama, baba wa kuletewa

**Na Beatrice Philemon,** aliyekuwa MAFIA



Huu ndio usafiri kati ya kisiwa cha Mafia na pwani ya Dar es Salaam na Rufiji. **PICHA: MTANDAO.**

UNAPOZUNGUMZIA wanawake katika Wilaya ya Mafia, Mkoa wa Pwani kwa wajihi ni wenye furaha na ndoto za kupambana na umasikini.

Ukija upande wa pili, kizingiti kikuu kiko katika tatizo la usafiri kutoka Mafia hadi kisiwani Nyamisati, wilayani Rufiji na kutoka hapo hadi soko kuu la bidhaa zao, Mbagala-Dar es- Salaam.

Baada ya kupata elimu ya ujasiliamali kutoka shirika la ActionAid, jinsi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali hasa za nazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, hivi sasa wameanza kujitambua wakitengeneza bidhaa zitokanazo na nazi, hapo inajumuisha mafuta ya nazi ya mgando, mafuta ya nazi ya maji na losheni zake.

Wengine wanajikita kutengenezaji sabuni za mwani, na za maji, biashara ya samaki na bidhaa za mikono kama vile shanga, mikeka, vikapu.

Wapo kinamama wanaochukua hatua kusafiri hadi Dar es Salaam kutafuta bidhaa za kuziuza Mafia. Hapo ndipo, inaibuka kero ya usafiri inayorudisha juhudi zao Mafia.

### MWEZESHAJI AONGEA

Mwanaiman Abdallah, ni Mwezeshaji kutoka Sauti ya Wanawake Mafia (SAWAMA ), ni miongoni mwa walionufaika na elimu ya ujasiriamali kutoka ActionAid, kupitia mradi wa Local Right Programme (LRP) unaotekelezwa wilayani humo .

Mwanaimani anasema, LRP imewafunza kinamama jinsi ya kutunza fedha, kumbukumbu za biashara na kuongeza thamani ya mazao yao, elimu ya masoko, kutengeneza vitu bora na masoko yake.

Anasema, kujiamini kumewasaidia wanawake kujikita katika shughuli za kiuchumi inayowaongezea kipato na familia, taifa nalo linanufaika.

Mama huyo anasema wamefundishwa jinsi ya kubaini fursa na changamoto na elimu ya utawala bora. Mwanaimani, ambaye pia Mjumbe Mwezeshaji wa Mduara wa Wanawake wilayani Mafia, anasema ingawa elimu imewasaidia kutengeneza bidhaa mbalimbali, lakini bado hawanufaiki nazo kwa sababu ya adha ya usafiri.

Pia, suala la gharama kubwa za usafirishaji, ulipaji kodi na mengine yanayochangia kwa kiasi kikubwa wanawake Mafia kuendelea kuwa masikini na biashara zao kushindwa kukua.

Mbali na hilo, usafiri unaotumia kwa ajili ya abiria na mizigo ni hatari sana kwa maisha ya binadamu, wanatumia boti na majahazi, na asilimia kubwa ya boti na majahazi ni mabovu saa nyingine zinazima kati kati ya bahari kitu ambacho ni hatari sana kwa maisha ya binadamu, yaani inabidi watu waanze kusali ili Mungu awasaidie waweze kufika salama.

"Usafiri kutoka Mafia kwenda Dar es Salaam ni Shida na kutoka Nyamisati kuja Mafia, pia shida kwa sababu unaweza kukaa Nyamisati siku tatu hadi ukisubiri kupata usafiri kwa sababu boti na majahazi zilizopo eneo hilo ni mbovu sana," amasema

"Yaani unaweza kufika nyamisati hakuna boti kabisa, saa nyingine una watoto, lakini kutokana na ukosefu wa usafiri unaanza kutumia nauli ili kujikimu na kama ulienda Dar es Salaam kufanya biashara basi utaanza kutumia fedha za mauzo ili kujikimu mpaka utakapo pata usafiri," anasema

> **Kabla ya kujikita katika biashara hii, Mwanaimani alikuwa akifanya biashara ndogo ndogo ya kuuza ubuyu, kokoto na sambusa na fedha kidogo alizopata alitoa kiasi cha Sh. 12,000 kila wiki.**

Anasema kupitia elimu aliyoipata hivi sasa amekuwa mfanyabiashara anaenda katika mikoa mbalimbali, ikiwamo Dar es Salaam anakonunua nguo na kuja nazo Mafia kuu na anatoa huduma za Tigo Pesa. Fedha alizopata kupitia biashara hiyo, anasema amenunua ng'ombe wanne, viwanja viwili na mpaka sasa yuko katika hatua za ujenzi wa nyumba ya kisasa.

"Kabla ya kujikita katika biashara hii, Mwanaimani alikuwa akifanya biashara ndogo ndogo ya kuuza ubuyu, kokoto na sambusa na fedha kidogo alizopata alitoa kiasi cha Sh. 12,000 kila wiki na kuchangia kwenye Vikoba, ili kupata mtaji kwa ajili ya kupanua biashara yake ambayo anaifanya hivi sasa.

"Ingawa ActionAid Tanzania wamenifumbua macho wakiwamo wanawake wengine katika wilaya ya Mafia, changamoto yetu kubwa ni usafiri na soko la kuuza bidhaa zetu.Bidhaa zetu ni nzuri tena za asili akini bado watu wengi hawajafahamu," anasema na kulalamika wananchi wengi wa Mafia hawana uwezo wa kutumia ndege, kwa sababu ya gharama

### MDUARA

Mbali na tatizo la usafiri, hivi sasa kinamama hao wa Mafia wameanzisha kinachoitwa 'miduara' kwa ajili ya kuchambua changamoto zao na kuzitatua ili kuleta mabadiliko.

"Kupitia miduara hii hivi sasa wanawake wanajua changamoto zinazowakabili, wamejua haki zao na jinsi ya kuzitafuta. Watoto wa kike wameanza kupelekwa shuleni tofauti na miaka ya nyuma.

" Pia, mimba za utotoni na ndoa za utotoni zimepungua kwa kiasi kikubwa, baada ya wazazi kupata elimu ya athari za ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike," anafafanua Mwanaimani.

"Pia, hivi tunatafuta njia ya kujikomboa kwa kutumia mikutano ya hadhara ili kuhamasisha jamii na wanaume zetu majumbani, kuhusu ukatili wa kijinsia ili kubadili mfumo wa malezi na mfumo dume uliopo unaomkandamiza mwanamke na mtoto wa kike," anasema.

Anataja matarajio yao ni wanawake wawe na muda wa kupumzika na mabinti zaio kusoma. Mwanaimani anafafanua, wilayani Mafia mwanamke ndiye anayelisha familia na majukumu mengi, wanaume hawashughuliki."

Hivi sasa ukatili unaoongoza kwa wanawake katika Wilaya ya Mafia ni majukumu mengi kwa akina mama kufanya shughuli za kiuchumi, kuhudumia familia, kusomesha watoto, kutunza familia, kununua vifaa vya shule, shughuli za shamba, kuchota maji, kutafuta kuni,shughuli za nyumbani na pia baba kuwa tegemezi kwa mama.

Anasema, ndio dhana iliyozaa matukio ya ukatili wa kijinsia, miaka ya nyuma yakiwa mkubwa, ikiwamo ubakaji, kwa sababu mama anakuwa na muda wa kupumzika kuongea na wanawe.

Kabla ya 'miduara' asasi ya Sauti ya Wanawake Mafia (SAWAMA), anasema haikufahamika sana kwa kinamama, hivyo hawakuzijua haki zao za msingi kama vile mabinti kupata elimu sawa na wavulana, afya ya uzazi salama na hawakujua pa kushitaki wanapopigwa.

Anasema hivi sasa wanawake wa Mafia wamefumbuka macho na wameanza kujua haki zao, baada ya ActionAidTanzania kuanza kutoa elimu katika wilaya ya Mafia ili kusaidia wanawake na watoto kujua haki zao.

Hivi sasa wengi katika Wilaya ya Mafia wanajua haki zao ikiwamo elimu ya afya ya uzazi salama, athari za mimba za utotoni, wengi wameanza kufanya shughuli za ujasiriamali, wamejua umuhimu wa elimu na kuanza kusomesha watoto wao na pia wamefahamu sehemu ya kushitaki kama mtu akifanyiwa ukatili wa kijinsia tofauti na miaka ya nyuma.

UCHUMI

# Mbunge Maige adokeza wapi Veta inasimamia pengo ajira

• Nafasi ya mabinti; Veta Mwakata nao...



Wanafunzi Chuo cha Ufundi Mwakata, wakionyesha ujuzi wao katika kada ya ufundi cherehani. **Chini;** wakionyesha mfumo wa umeme unavyofanya kazi. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VYUO vya Maendeleo ya Ufundi Stadi maarufu 'Veta' vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini, vimekuwa vikichangia kwa asilimia kubwa kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana na hasa mabinti, waliomaliza elimu ya msingi na sekondari na hawajapata mwelekeo wa kimaisha, ikiwamo ajira.

Veta inatoa mafunzo ya stadi na fani mbalimbali, wengi ni wale waliomaliza elimu msingi na kidato cha nne na hawakufanikwa kuendelea na ngazi za juu. Ni mtazamo unaoenda mbali, hata kwa wale walioko mitaani kwa sababu moja na nyingine 'wanaelea.'

Aidha, Veta imekuwa ikitengeneza wataalamu mbalimbali na kuna wakati inawatoa walio bora zaidi kuliko hata waliofika vyuo vya juu zaidi katika stadi hizo.

Kwa mabinti, wamekuwa wakipewa ujuzi katika stadi kama utumiaji vyerehani, mitindo, udereva, upishi na umeme, vyote vikiwasaidia kupunguza wimbi la wasichana kutojihusisha na uuzaji miili yao, kama namna ya kujikimu kimaisha.

**MBUNGE MSALALA**

Ezekiel Maige, ni Mbunge wa Jimbo la Msalala, anasema kuwa, vyuo vya ufundi vimekuwa vikichangia kwa kiwango kikubwa kupunguza wimbi la vijana mitaani wasiokuwa na ajira kwa kujiajiri kutokana na fani waliyoipata kwenye vyuo hivyo.

Pia, anasema vimepunguza wimbi la vijana kutojihusisha na uhalifu, vijana wengi wanaomaliza elimu, mbali na wachache wanaoingia katika uhalifu, bado vijana wanajihusisha ama kwenye ufugaji au kilimo kisicho na tija.

> **Katika kukabili changamoto ya ajira zao, wanatarajia kuanzisha fani za ufugaji na kilimo, sambamba na vikundi vya ujasirimali vinavyoendana na fani zao, waweze kujiajiri wanapohitimu.**



Anasema, wamekuwa wakitumia nguvu kubwa katika kuandaa mashamba, lakini wanaishia katika mavuno kidogo na wapo wanaokata tamaa, ilhali endapo wangepata elimu ya kilimo wangepata hatua kubwa ya mafanikio, hata kuwa wakulima wakubwa.

"Vyuo vyetu vya ufundi kwa kiwango kikubwa vimepunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Wanahitimu elimu ya msingi na sekondari na kukosa alama za kuendelea na masomo na wanaanza kuranda mitaani, kusubiri kulelewa na wazazi wakijiingiza kwenye vitendo vibaya," anasema Maige.

**UFUGAJI SAMAKI**

Maige anawataka wasimamizi wa vyuo vya ufundi kuanzisha mafunzo ya ufugaji wa samaki, nguruwe, ng'ombe wa maziwa na kilimo, ili wanavyuo hao waweze kujikita katika mazingira ya kilimo chenye tija na ufugaji wa kisasa.

Anasema, kuna vijana wanaosomea fani za umeme au udereva wa magari na wamekuwa wakikosa nafasi za kuonyesha ujuzi wao ndani ya jamii, shida kuu ni kukosa sifa za kupata ajira, kulingana na alama alizozipata kwenye mitihani yake ya mwisho.

"Kila mtu anaenunua gari, anafahamu kuendesha vizuri tofauti na kipindi cha nyuma, walikuwa wakitafuta madereva wa kuwaendesha. Hii ni kuogopa kuingia kwenye gharama, ni vyema tukaanzisha fani za ufugaji samaki, nguruwe, ng'ombe wa maziwa na kilimo cha kisasa ili wajikite huko," anasema Maige.

**MIKOPO/UJASIRIMALI**

Anasema, wasimamizi wa vyuo vya ufundi wanatakiwa kuanzisha vikundi vya ujasiriamali kwa wanavyuo na kuwapatia mikopo itayowapa mitaji, pindi vijana wanapohitimu masomo, lengo ni kujiajiri.

Maige anasema, sehemu kubwa ya wanavyuo wameshindwa kujiajiri, kutokana na ukosefu wa mitaji na badala yake wanahamisha maisha 'vijiweni' na kuranda mitaani, wakianza kuwa wanachama wa vikundi visivyofaa.

"Tuna vijana wengi mitaani wamemaliza vyuo vya ufundi, lakini wameshindwa kujiajiri kwa kukosa mitaji. Ili waweze kujiajiri kulingana na fani zao, tunatakiwa kuanzisha vikundi vya ujasirimali, ambavyo vitakopeshwa na halmashauri na chuo kitakuwa mdhamini wao," anasema Maige.

"Halmashauri zimekuwa zikitoa mikopo yenye riba nafuu kwa vikundi vya wajasirimali na kinamama, vijana na watu wenye ulemavu na wengi wanaopewa mikopo hiyo, hawana elimu ya kile wanachoendea kukifanya, kama ambavyo wangepatiwa wanavyuo vya ufundi," anaongeza.

**MKUU UFUNDI MWAKATA**


Padre Jose Eriyanicka, ni mwanzilishi wa Chuo cha Ufundi Mwakata (S.F.S VTC) kilichopo katika Kata ya Mwakata, ndani ya Halmashauri ya Msalala, anasema mbali na kutoa ujuzi wa fani za kifundi, pia wanatoa ajira kwa vijana wanaofanya vizuri masomoni, wanaokuwa walimu.

Anasema katika kukabili changamoto ya ajira zao, wanatarajia kuanzisha fani za ufugaji na kilimo, sambamba na vikundi vya ujasirimali vinavyoendana na fani zao, waweze kujiajiri wanapohitimu.

Padre Jose anasema hadi sasa wamekwama kuanzisha fani za ufugaji samaki na ng'ombe wa maziwa, nguruwe na kilimo kwa sababu hawana vyanzo bora na maji ya uhakika, kwani maji wanayoyatumia, wanayatoa umbali wa kilomita 10, yakisombwa na magari.

Anafafanua kwamba, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, umepita nyuma ya chuo hicho ukielekea Kata ya Isaka na endapo watauganishiwa maji hayo, itakuwa rahisi kuanzisha fani hizo tajwa, wanavyuo kujifunza kwa vitendo na nadharia.

Mratibu Mafunzo wa chuo hicho, Charles Maganga, anasema, zaidi ya wanavyuo 177 wamehitimu fani mbalimbali na wengine tisa walisitisha masomo kutokana na ukosefu wa ada, utovu wa nidhamu.





Mbunge wa Jimbo la Lupa, mkoani Mbeya, Victor Mwambalaswa (wa pili kushoto), ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya mkoa huo, akizungumza kwenye kikao cha kamati hiyo, kilichofanyika, jijini humo juzi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC aagiza taasisi za serikali kukatiwa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameuagiza uongozi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mbeya-WSSA) kuzikatia huduma ya maji taasisi zote za zerikali zinazodaiwa madeni ya ankara.

Alitoa agizo hilo juzi kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichofanyika mjini Mbeya na kuagiza ukataji wa huduma hiyo ufanyike Desemba 15, mwaka huu. Baadhi ya taasisi zilizo hatarini kukumbwa na kadhia hiyo ni Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambayo baadhi ya taasisi zake, zikiwamo shule, zitaathirika.

Chalamila alisema atamshtaki Mkurugenzi Mtendaji wa mamlaka hiyo kwenye mamlaka za juu endapo hatatekeleza agizo hilo ili atumbuliwe kwa kuwa, baadhi ya maeneo wananchi wanalalamika kukosa huduma hiyo kutokana na miundombinu kuchakaa.

Alisema taasisi hizo zingelipa madeni yake yanayofikia Sh. bilioni nne, huduma ya maji ingeboreshwa zaidi ndani ya mkoa huo na kusisitiza hatanii anapoagiza kukata huduma hiyo.

"Kesho (jana) niandikie barua uniainishie madeni ya kila taasisi, lakini pia ziandikie barua kuzitaarifu kuwa Desemba 15 zitakatiwa huduma na mimi nitaziandikia kutahadharisha, kama ni waziri anatakiwa kulipa, alipe na kama ni Kamishna wa Magereza alipe," aliagiza.

Alisema ukataji wa huduma hiyo pia ufanyike dhidi ya wananchi wanaodaiwa na ikiwezekana vyombo vya dola vitumike kuwalazimisha kulipa ili mamlaka ijiendeshe na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Awali, akitoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa majisafi mkoani Mbeya, Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Ndele Mengo, alisema taasisi hizo zinadaiwa madeni makubwa na zimekuwa nzito kulipa. Alizitaja taasisi hizo kuwa ni pamoja na vituo vya afya, taasisi za elimu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya ambazo zinadaiwa zaidi ya Sh. milioni 100.

Taasisi zingine alizozitaja ni vyombo vya dola ambavyo ni JWTZ linalodaiwa Sh. milioni 43.9, Jeshi la Polisi na vitengo vyake Sh. milioni 657.9 na Jeshi la Magereza, lenye deni kubwa zaidi la Sh. milioni 631.9 huku chuo chake (Chuo cha Magereza) kikidaiwa Sh. milioni 225.8. "Madeni haya yanatusumbua kwa muda mrefu, hizi taasisi zimekuwa nzito sana kulipia ankara, sasa tunaomba serikali itusaidie, baadhi ya maeneo huwa tunatakiwa kufanyia maboresho miundombinu, lakini tunashindwa kwa sababu pesa hazipo," alisema.

Aliongeza kuwa upatikanaji wa majisafi jijini Mbeya umefika asilimia 89.9 na kwamba bado wanaona kuna upungufu ambao utazibwa na miradi inayoendelea kutekelezwa ndani ya mkoa, ukiwamo wa Mbalizi.

Aliwataka wananchi kuendelea kulipia huduma hiyo ili kuiwezesha mamlaka hiyo kujiendesha na kuboresha miundombinu ambayo imechakaa.

# Teknolojia duni yaponza wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa viazi mkoani Mbeya wanapoteza zaidi ya asilimia 40 ya mazao yao kutokana na matumizi ya teknolojia duni kwenye uvunaji na kutokuwa na elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, wakati wa kikao cha wadau wa viazi mviringo mkoani wakiwamo wakulima, watafiti na wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV).

Alisema wakulima wengi mkoani humo wanatumia nguvu na rasilimali nyingi wakati wa kuzalisha, lakini wanaambulia mavuno kiduchu. Alisema mazao yao mengi yanabaki kwenye ardhi wakati wa mavuno, hivyo kuingia hasara na baadhi yao kukata tamaa ya kuendelea na kilimo hicho.

Madito alisema baadhi ya wakulima hupoteza mazao yao kutokana na kutozingatia muda sahihi wa kuvuna, akifafanua zaidi kuwa wengi huchelewa kuvuna, hivyo kusababisha mizizi inayoshikilia viazi kuoza.

"Baadhi wanatumia majembe ya mkono wakati wa kuvuna, hali ambayo husababisha waache viazi vingi kwenye udongo, lakini pia matumizi ya jembe la mkono husababisha majeraha kwenye viazi na hivyo kutokuwa na soko," alisema. Aliongeza kuwa viazi vilivyokatwa havikai muda mrefu sokoni kwa maelezo kuwa huwa vinaoza mapema, hivyo akawataka wakulima kuwa makini wakati wa kuvuna.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo waliohudhuria kikao hicho, walikiri mavuno yao kushuka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na matumizi ya teknolojia duni katika uvunaji.

Mmoja wa wakulima hao, Ibrahim Lyamos, alisema awali alikuwa anapata magunia 40 mpaka 50 kwa ekari moja, lakini sasa anapata wastani wa magunia 30 kwa ekari. "Tunaomba serikali na wataalamu mbalimbali waendelee kutupatia elimu bora ya kilimo ili angalau tuondoke kwenye kiwango hicho cha mavuno, sisi tunalima kilimo duni mno," alisema.

Shirika la SNV limeanzisha mradi maalum wa miaka mitano wa kuwakwamua wakulima kutoka kwenye mavuno duni.

Ofisa Kilimo wa SNV, Godfrey Kahabuka, alisema mradi huo unalenga kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kushirikiana na wadau wengine ili wakulima waongeze uzalishaji. Alisema wanashirikiana na wazalishaji wa mbegu ili wazalishe mbegu ambazo zinakabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na wasambazaji wa pembejeo zingine zikiwamo mbolea na dawa za wadudu.

# NEC yavipa neno vyama vya siasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imevitaka vyama vya siasa nchini kuzitumia kamati za maadili na mamlaka zingine za usimamizi wa uchaguzi ili kutatua matatizo yanayojitokeza katika uchaguzi badala ya kukimbilia kwenye vyombo vya habari.

Imesema utaratibu wa baadhi ya vyama kukimbilia kwenye vyombo vya habari kulalamika kunapotokea dosari katika uchaguzi, hauna mashiko kwa kuwa havina mamlaka za kisheria kushughulikia matatizo hayo.

Akizungumza wakati wa mkutano wa wadau wa uchaguzi mkoani Mbeya juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wamekuwa wakikiuka taratibu kwa kukimbilia kwenye vyombo vya habari.

Alisema mtu yeyote ambaye haridhishwi na mwenendo wa uchaguzi anatakiwa akate rufani kwenye kamati ya maadili na kama bado ataona kuwa hakutendewa haki ni vema akakata rufani kwenye kamati za rufani ambazo zinakuwa na uwakilishi wa wadau wote. Alisema tatizo la wanasiasa kutoa malalamiko yao kwenye mamlaka ambazo hazihusiki, limebainika zaidi kwenye uchaguzi mdogo, akieleza kuwa wengi walikimbilia kwenye vyombo vya habari kueleza dosari zilizojitokeza.

"Baadhi ya wanasiasa wameonekana kutoziamini hizi kamati za maadili ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria, sasa wanakimbilia vyombo vya habari na baadhi ya vyombo hivyo badala ya kuleta amani, vinachochea kutoweka kwa amani," alisema. Alivitaka vyombo vya habari kuacha kufanya kazi visiyoruhusiwa kisheria na badala yake, viwashauri wahusika kwenda kwenye kamati za maadili.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa waliohudhuria mkutano huo, waliiomba tume hiyo kutenda haki kwa vyama vyote wakati wa uchaguzi badala ya kukipendelea chama tawala. Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Wilaya ya Mbeya Mjini, John Mwambigija, alidai katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 24, vyama vya upinzani havikutendewa haki. Alisema vyama hivyo vilitengwa katika uchaguzi huo na baadhi ya watu ambao wamepewa mamlaka kwa lengo la kukisaidia chama tawala kupita bila kupingwa.

"Baadhi ya watu ambao walitakiwa watusaidie ndiyo hao walikuwa wanatukimbia, tulikuwa tukienda kwenye ofisi za watendaji wa mitaa tunakuta wamefunga ofisi, sasa na hao ndiyo waliopewa mamlaka ya kusimamia zoezi hili," alisema.

Akifungua Mkutano huo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alisema kabla ya kuanza kwa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, tume imefanya tathmini na kujiridhisha kuwa mashine za kielektroniki za kusajili wapigakura (BVR) zina uwezo mkubwa.

Alisema mashine hizo zina uwezo wa kuwawezesha wapigakura kupata kadi zao kwa wakati na kwa usahihi endapo watakuwa wametoa taarifa sahihi.



HABARI DODOMA

# Wakulima kusajiliwa kwa mfumo maalum

**Na Faustine Feliciane,** DODOMA

SERIKALI imeandaa utaratibu wa kuwasajili wakulima wote nchini na kutambua kilimo wanachokifanya.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kongamono la kilimohai, kwa kuwa utaratibu huo utasaidia kujua idadi yao nchini.

"Wapo wanaojiita wakulima lakini hakuna kilimo wanachokifanya, tunataka kuwa na kanzi data ya wakulima nchini na tujue kilimo wanachokifanya," alisema Hasunga.

Alisema serikali inatambua jitihada za wakulima hasa wale wanaolima kilimohai, ambacho mazao yake yanahitajika zaidi kwa ajili ya kuokoa afya za watu.

"Kwa sasa serikali inaweka fedha nyingi kwenye afya kutokana na kuwapo na magonjwa mengi ambayo yanayotokana na ulaji wa vyakula vinavyozalishwa kwa kemikali za viwandani," alisema.

Waziri huyo alisema kama watu watalima kilimohai kwa njia ya asili watausepusha jamii na magonjwa na kuipunguzia mzigo serikali.

Alisema serikali itakuwa karibu na wakulima wa kilimohai kuhakikisha kilimo hicho kinaendelezwa kwa manufaa ya wananchi.

Hasunga alisema serikali itaanzisha kitengo maalum cha kilimohai kwenye wizara hiyo na kuweka kurugenzi itakayofanya kazi na kufuatilia kwa karibu kilimo hicho.

"Serikali inalipongeza Shirika la Kuendeleza Kilimohai Tanzania (TOAM) kwa kuendeleza kilimohai kwa kuwa karibu na wakulima na kutoa mafunzo mbalimbali," alisema.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kushoto), akijadiliana jambo na wageni waliohudhuria uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia mkoani Dodoma juzi. Katikati ni Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Wakili Anna Kulaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu walia na miundombinu

**Na Peter Mkwavila,** KONDOA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (Shivyawata) Mkoa wa Dodoma, limeiomba serikali kuhakikisha maeneo yanayotoa huduma muhimu za kijamii yana miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Katibu wa Shirikisho hilo Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu yatakayofanyika Desemba 3, mwaka huu. Alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na mahakamani, hospitalini na maeneo mengine ambayo hayana miundombinu rafiki na wataalamu wa lugha.

"Hata mikutano tunakosa wataalamu wa kutusaidia kisiasa hivyo tunakosa haki ya msingi ya kusikia na kuelewa yanayosemwa kwenye mikusanyiko," alisema.

Kuhusu maadhimisho hayo, katibu huyo alisema yatafanyikia halmashauri ya mji wa Kondoa ambako kutakuwa shughuli na mbalimbali za kijamii kama vile kufanya usafi Hospitali ya Wilaya ya Kondoa, kutembelea wodi ya kinamama na watoto pamoja na shule ya msingi Iboni inatoa elimu jumuishi ili kutoa msaada.

Aidha, alisema kutakuwa na kongamano la kujadili changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo watu wenye ulemavu katika kupata haki zao za msingi. Mmoja wa wakazi wa Dodoma, Juliana Mathayo, alisema bado kuna tabia ya kuficha watoto wenye ulemavu badala ya kuwapeleka shule na kwamba kupitia maadhimisho hayo viongozi wa serikali watatoa elimu ya kutosha.

Mathayo alisema wananchi watapata elimu ya umuhimu wa mtoto mwenye ulemavu na kutambua kuwa wanatakiwa kupata haki sawa na watoto wengine.

## Halmashauri zafundwa kuhusu mipango endelevu

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

HALMASHAURI zimetakiwa kuwa na mipango inayotekelezeka kwenye utoaji wa elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi, ili kuwafikia wakulima katika maeneo yao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, alisema hayo jijini hapa juzi wakati akifungua mkutano wa wadau wa kilimo kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo ulioandaliwa na Jukwaa Lisilo la Kiserikali la Wadau wa Kilimo (ANSAF), pia ulijadili fursa zilizopo katika sekta ya kilimo na utayari wa nchi katika kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Waziri huyo alisema upo umuhimu wa kuwajengea uwezo maofisa ugani kutekeleza jukumu hilo muhimu pamoja na kuboresha mawasiliano na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ili wananchi wapate taarifa na kulima mazao kulingana na hali ya hewa kwa wakati husika.

Simbachawene alisema mabadiliko ya tabianchi ni tishio duniani, ikiwamo Tanzania ambayo athari zimeonekana kwenye mabadiliko ya msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame na mafuriko ya mara kwa mara.

Nyingine ni ongezeko la wadudu waharibifu na magonjwa yasiyosikia dawa ya mimea na wanyama, ambavyo vimesababisha wakulima wengi kutopata mavuno ya kutosha na yaliyotarajiwa.

"Pia wanawake na vijana wameonekana kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na ukosefu wa nyenzo za kisasa za kilimo, elimu, kipato kidogo na kushindwa kumiliki ardhi ingawa ndio wenye kufanya kazi kubwa ya uzalishaji," alisema na kuongeza.

"Tunaona uharibifu wa vyanzo vya maji husababisha mama zetu na mabinti zetu kutembea umbali mrefu kusaka maji, hii inaweka usalama wao katika mazingira hatarishi na kaya zinapokosa chakula cha kutosha kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, wanawake na watoto ndio waathirika wakuu," alisema.

Aidha, aliwataka wadau wa maendeleo kuhakikisha mbinu zinazotumika katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinakuwa shirikishi na zinazingatia ushiriki thabiti wa wanawake na vijana.

"Kuwepo na mikakati kabambe ya kulikwamua kundi hili na changamoto hii kama vile uchimbaji wa visima katika maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa vyanzo vya maji vimekauka kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Alitoa wito kwa wadau wengine kushauriana namna bora ya kusaidia jamii kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ili miradi ya kilimo istahimili mabadiliko hayo.



## HABARI ZANZIBAR

# Wanawake wataka nafasi Baraza la Maulamaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametaka muundo wa Baraza la Maulamaa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kutekeleza majukumu yake vizuri kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto za wanawake.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema jana wakati akichangia muswada huo na kutaka muundo mpya, kuingiza wajumbe wanawake.

Alisema hivi sasa jamii ya wananchi wa Zanzibar wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kuporomoka kwa maadili pamoja na udhalilishaji wa kijinsia yakiwamo matukio ya ubakaji, ulawiti na mimba kwa wanawake chini ya umri wa miaka 18. "Matukio yote hayo yanahitaji mchango mkubwa wa wanawake ambao wataingia katika Baraza la Maulamaa ili kusaidia kupatikana kwa ufumbuzi wake," alisema.

Kauli ya Mgeni imekuja baada ya kubainika kwamba hakuna kifungu cha sheria katika muswada wa Ofisi ya Mufti unaotaja kwamba Baraza la Maulamaa lenye jukumu la kutoa 'fatwaa' kwa upande wa dini ya Kiislamu, hakuna wajumbe wanawake. Naye Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, ambaye ni Waziri asiye na Wizara Maalumu, Said Soud, alipinga wanawake kuingizwa katika Baraza la Maulamaa na kusema ni kwenda kinyume cha misingi ya dini ya Kiislamu.

Alisema katika zama za kiongozi wa dini ya Kiislamu Mtume Muhamad mwanamke hakupewa kipaumbele cha kuongoza ikiwamo kuwa imamu kwa waumini wengine.

"Sheria hii ni muhimu kwa sababu inakwenda sambamba na maelekezo ya dini ya Kiislamu ambalo baraza la maulamaa ni daraja kubwa la kutoa fatwa katika masuala ya dini ya kiislamu"alisema.

Akijibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia muswada wa marekebisho ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti, Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, alikitaja kifungu cha 11 A kwamba hakijakataza na kuwanyima haki wanawake kuingia katika Baraza la Maulamaa.

Alisema si lazima kuwapo kipengele ambacho kitataja moja kwa moja kuhusu wanawake kuingia katika Baraza la Maulamaa.

Alieleza kuwa Mufti anao uwezo wa kuwaalika wanawake katika baraza hilo kwa ajili ya kupata ushauri au ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu wanawake. Aidha, alisema kwamba asilimia 95 ya wajumbe wa Baraza la Maulamaa wanaingia katika baraza kwa mujibu wa nyadhifa zao. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipitisha marekebisho ya Sheria Na. 9 ya mwaka 2001 ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti Zanzibar.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Said Hassan Said, alisema Ofisi ya Mufti majukumu yake ni makubwa ikiwamo kusimamia masuala ya Waislamu ikiwamo ndoa,talaka na masuala ya urithi na mgawanyo wa mali.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar, Said Hassan (kushoto), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Shamsi, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, huko Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Zanzibar yajivunia ugatuzi madaraka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwapo kwa mfumo wa ugatuzi kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha huduma za maendeleo vijijiji ikiwamo ujenzi wa barabara za ndani.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, Shamata Shaame Khamis, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu Pemba, Bihindi Khamis Hamad, aliyetaka kujua barabara ngapi zimejengwa tangu kuanza kwa ugatuzi.

Shamata alisema barabara tisa zimejengwa ikiwamo ya kiwango cha lami kwenda vijijini, hivyo kusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa shughuli za maendeleo ikiwamo sekta ya kilimo.

Alisema kwa upande wa Pemba, Wilaya ya Chake Chake, barabara ya Msingini na ile inayokwenda katika Ofisi ya Tume ya Uchaguzi (ZEC) imefanyiwa ukarabati mkubwa.

Pia alizitaja barabara za Unguja ikiwamo ya Kikwajuni hadi Fuoni Mambosasa kuwa ni sehemu ya barabara ambazo zimefanyiwa matengenezo na halmashauri ya tawala za mikoa.

Alisema hayo ni sehemu ya matunda ya kuwepo kwa mfumo wa ugatuzi ambao lengo lake ni kufikisha huduma muhimu za kijamii kwenda kwa wananchi moja kwa moja.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza mpango wa ugatuzi katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2017/18 na tayari sekta tatu zimegatuliwa.

Taasisi zilizogatuliwa ni elimu ya maandalizi na msingi, sekta ya afya ya msingi pamoja na idara ya kilimo.

# Utaratibu hotuba Ijumaa misikiti yote kuandaliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, amesema Ofisi ya Mufti itaangalia utaratibu wa kutayarisha hotuba za Ijumaa na kusomwa katika misikiti yote tofauti na sasa kila msikiti unakuwa na utaratibu wake.

Mwalimu alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chake Chake Suleiman Sarhani, aliyetaka kujua kwa nini hadi sasa hakuna utaratibu wa Ofisi ya Mufti kutayarisha hotuba za Ijumaa na kusomwa na maimamu katika misikiti yote.

Alikiri na kusema ni kweli kwamba hadi sasa hakuna utaratibu wa aina hiyo wa Ofisi ya Mufti kutayarisha hotuba moja itakayosomwa katika misikiti yote.

Alisema ni vizuri kuwapo kwa utaratibu huo ambao hotuba za Ijumaa hutayarishwa na kubeba ujumbe unaoendana na hali halisi ya nchi.

Mwalimu alisema baadhi ya misikiti, maimamu wake hutayarisha hotuba ambazo zingine imebainika kuhatarisha amani ikiwamo kauli za chuki dhidi ya viongozi wakuu wa nchi.

"Suala hilo tutalitafakari na kulifanyia kazi.

Ni muhimu kuwapo kwa hotuba za sala ya Ijumaa ambazo zinatayarishwa na Ofisi ya Mufti ili zitoe ujumbe unaokwenda sambamba na hali halisi ya nchi," alisema.

Waziri alisema sheria ya mufti inatoa nafasi ya kushughulikia masuala yote yanayohusu mambo ya misikiti ikiwamo matayarisho ya hotuba za sala ya ibada ya Ijumaa.

Sala ya Ijumaa miongoni mwa masharti yake ni kusaliwa katika siku ya Ijumaa si chini ya watu 40 wenye akili timamu na husomwa hotuba mbili zenye muktadha wa mambo mbalimbali yanayoikabili jamii na kutowa ujumbe wake.

# TCU yasisitiza vyuo ubora wa elimu

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

KATIBU Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, amevitaka vyuo vikuu nchi kuzingatia ubora wa elimu ili kuepusha usumbufu kwa wanafunzi kushindwa kumaliza masoma kutokana na vyuo hizo kukosa vigezo vya ubora.

Alisema mwaka jana kuna baadhi ya vyuo ambavyo vilifutiwa usajili na TCU kwa kushindwa kukidhi vigezo vya ubora, hivyo kusababisha usumbufu kwa wanafunzi kuhangaika kwa ajili ya hatima yao ya baadaye.

Prof. Kihampa alisema hayo katika mahafali ya 11 ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema jumla ya wanafunzi 2,600 mwaka jana walihamishiwa kutoka katika vyuo vikuu mbalimbali nchini baada ya vyuo hivyo kufutiwa usajili na TCU kwa kukosa sifa.

Alisema kati ya wanafunzi 2,600 wapo wanafunzi 341 kutoka Chuo Kikuu cha Ekonford cha Tanga waliohamia MUCE, na katika mahafali hayo jumla ya wanafunzi 99 walihitimu masomo yao kutunukiwa stashahada za uzamili na shahada za awali.

Alisema hakuna mwanafunzi ambaye amebaki nyumbani baada ya vyuo vyao kufutiwa usajili na TCU, kwa sababu za kushindwa kukidhi vigezo vya ubora.

Alizitaja baadhi ya sababu zilizosababisha vyuo vikuu vingi nchini kufutiwa usajili ni changamoto ya rasilimali fedha ambapo imesababisha vishindwe kuwalipa wahadhiri.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam UDSM, Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, alitunuku stashahada ya uzamili na shahada kwa wanafunzi 1,275.

Wakizungumza na waandishi wa habari wakati wa mahafali hayo, wanafunzi wao walipongeza serikali kwa kusimamia ubora wa elimu ya juu nchini.

Aliyekuwa Rais wa serikali ya wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Ekenford Tanga, Micheal Mbezi, aliipongeza serikali kwa kusimamia viwango vya elimu inayotolewa kwenye taasisi za elimu ya juu nchini.

Alisema kuwa baadaye ya chuo chao cha Ekenford kufutiwa usajili serikali iliwapeleka wanafunzi 341 MUCE na kuendelea masomo katika hatua mbalimbali, ambapo asilimia 99 ya wanafunzi hao wamemaliza masomo yao na kutunikiwa stashahada ya uzamili na shahada.

Gladness Mshana, ambaye aliyehamia MUCE kutoka Ekenford, alisema wana kila sababu ya kuipongeza serikali kwa usimamizi wa karibu kwenye masuala ya elimu hasa katika kipindi hiki ambacho kumekuwa na utitiri wa taasisi za elimu ya juu nchini.

Kwa upande wake, Mkuu wa MUCE, Prof. Esther Dungumaro, alisema katika mwaka wa masomo 2018/2019 chuo kilipokea wanafunzi 341 kutoka Chuo Kikuu cha Ekenford cha Tanga baada ya chuo hicho kufutiwa usajili na TCU.

Alisema kati ya wanafunzi 341 waliohamia, wanafunzi 139 walifaulu na kuingia mwaka wa tatu kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Alieleza kwa wanafunzi 202 walipaswa kusoma masomo ya mwaka wa pili ili kukidhi viwango vya ubora vya mitaala ya chuo cha MUCE.



Vijana wakishusha mkaa kutoka kwenye lori ili kujipatia kipato cha siku nje ya soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Halmashauri yalia kushuka kwa mapato

**Na Anthony Gervas,** MAGU

UKUSANYAJI wa mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, umeshuka kutoka asilimia 90 hadi asilimia 70 kwa mwaka huu.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Elisha Hilal, alisema hayo juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani wakati wa kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi za robo ya pili 2019.

"Haiwezekani mapato yetu ya Halmashauri ya Wilaya yakashuke kwa kiasi hicho kutoka asilimia 90 hadi asilimia 70, halmashauri sasa tuna hali mbaya sana, yawezekana watendaji wanapuliza fedha hizo, nataka waliosababisha kushuka wakae pembeni," alisema Hilal.

Hilal aliwataka watendaji, wakuu wa idara na maofisa tarafa kushirikiana katika kusimamia ukusanyaji wa mapato hayo kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi badala ya kukaa maofisini tu.

"Kama mnashindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato hayo, hasa katika Kata ya Kisesa kwenye mradi wa mchanga kwa wenye malori, basi nikasimamie mimi," alisema na kuongeza: "Mwenyewe niwe nahesabu malori yanayosomba mchanga huo."

Alisema haiwezekani kata ya Kisesa, kukusanya Sh. milioni mbili au tano kwa mwezi, na kuitaka kamati ya fedha na wakuu wa idara kuwajibika kujibu hoja ya kushuka kwa mapato hayo katika vikao vijavyo vya baraza hilo.

Katibu Tawala Msaidizi wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Mwanza, Christina Bigambo, aliitaka halmashauri hiyo, kutekeleza miradi ya wananchi katika asilimia 40 inayotakiwa na serikali katika miradi ambayo ni viporo vya nyuma iliyokuwa imebaki bila kutekelezwa.

"Pamoja na halmashauri yenu kukusanya mapato, lakini mnatakiwa kuchangia asilimia kumi ya kinamama, vijana na wenye ulemavu. Asilimia 40 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ilibaki nyuma bila kutekelezwa na sio kuendelea na mipya," alisema Bigambo.

Bigambo alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Lutengano Mwalwiba, kufuata taratibu za utekelezaji wa miradi hiyo iliyolengwa katika asilimia hizo, vinginevyo atawekwa kitimoto tena kama kipindi kilichopita.

## Waziri: Vijana wafunzwe maadili, mila na desturi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, ametoa wito kwa wadau mbalimbali katika jamii kujitokeza kuandaa matamasha ya kufundisha vijana kuhusu maadili, mila na desturi nzuri.

Shonza ametoa wito huo jana, wilayani Mbulu alipokuwa akifunga Tamasha la Nne la Utamaduni na Michezo la Jamii ya Wairaiq lililenga kutoapiga vita mila potofu na kutoa hamasa kuwafundisha vijana wa jamii hiyo maadili, mila na desturi za jamii hiyo ili waweze kuzitunza na kuzienzi.

Naibu Waziri huyo aliwataka vijana wa jamii hiyo kuhakikisha wanazingatia malengo ya tamasha hilo ikiwamo kuzingatia suala la uwajibikaji na kuchapa kazi pamoja na kuacha masuala ya ulevi.

"Kila jamii katika taifa letu ikijipanga kufanya tamasha kama hili la utamaduni kwa vijana hakika tutajenga taifa bora lenye nidhamu, uwajibikaji na wachapakazi na hii itasaidia sana kupunguza wahalifu katika jamii yetu," alisema Shonza.

Pia Naibu Waziri huyo aliupongeza kwa uongozi wa Kanisa Katoliki Wilaya ya Mbulu kwa kuandaa tamasha hilo lenye tija kwa vijana ambao ndiyo taifa la kesho pamoja na Redio Habari Njema inayosimamiwa na kanisa hilo kwa kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii ikiwamo mila na desturi.

Kwa upande wake, Mhasham Askofu wa Jimbo Katoliki Mbulu, Mhashamu Anthony Lagweni Gaspar, aliiomba serikali kuanzishwa kituo cha kutunzia kumbukumbu za kimila na kuhifadhi zana mbalimbali za jadi vikiwamo vifaa vya muziki wa asili kama marimba.

"Kuwapo kwa kituo kinachoelezea historia, utamaduni, mila na desturi za watu wa jamii ya Kiiraiq katika wilaya hii kutasaidia kuongeza mapato kupitia watalii na kutangaza asili ya jamii hii pamoja na umahiri wa watu wake katika mchezo wa riadha,'' alisema Askofu Gaspar.

Halikadhalika askofu huyo aliendelea kusema kuwa kupitia tamasha hili tunapenda kukemea fikra za vijana za kuto wajibika na badala yake kusubiri kurithishwa mali za wazazi tunataka vijana waache uvivu na zaidi wajitume kutafuta mali zao wenyewe badala ya kutegemea mali za wazazi.

Naye Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay, alishukuru uongozi wa Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo kwa juhudi kubwa wanayofanya ya kusimamia masuala ya michezo na utamaduni kwa sasa.

## HABARI KIMATAIFA

# Benin yamtimua Balozi wa Umoja wa Ulaya

**COTONOU,** Benin

SERIKALI ya Benin imempa Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini humo, Oliver Nette, muda wa siku mbili hadi Jumapili Desemba Mosi awe ameondoka nchini humo.

Msemaji wa serikali ya nchi hiyo ya Afrika Magharibi, Alain Orounla (pichani chini), alisema jana kuwa balozi huyo kutoka Ujerumani alikuwa amejihusisha katika vitendo vya kuihujumu Benin.

Mwanadiplomasia wa ngazi ya juu katika nchi hiyo, alisema Balozi Nette mara kwa mara amekuwa akizihamasisha asasi za kiraia kufanya maandamano dhidi ya serikali ya nchi hiyo.

Tangu uchaguzi wa bunge wa mwezi Aprili, Benin imekumbwa na mfululizo wa maandamano, huku Rais wa nchi hiyo, Patrice Talon, akishutumiwa kuanzisha utawala wa kiimla.

Umoja wa Ulaya ni mfadhili mkuu wa Benin kifedha. **DW**



# Waandaanaji DRC wapinga mauaji ya maofisa ebola

**KINSHASA,** DR-Congo

WANAHARAKATI kutoka makundi ya kupigania haki za kibinadamu la Lucha na Operesheni Filimbi, wameandamana katika mji wa Goma katika ofisi ya ujumbe wa Umoja wa Mataifa (UN), Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo kupinga mauaji dhidi ya wafanyakazi watatu wa matibabu ya ebola.

**Miongoni mwa watu waliouawa ni wafanyakazi wa WHO na watu wengine wanne wamejeruhiwa vibaya.**

Waasi hao jana alfajiri walivishambulia vituo viwili vya matibabu vya ebola vinavyoendeshwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), katika uvamizi uliofanyika usiku wa kuamkia Alhamisi na kuwaua wahudumu watatu. Taarifa zinaeleza kuwa miongoni mwa watu waliouawa ni wafanyakazi wa WHO na watu wengine wanne wamejeruhiwa vibaya.

Kwa mujibu wa mashuhuda, waasi waliwazidi nguvu polisi kwenye vituo hivyo vilivyopo katika maeneo ya Mangina na machimbo ya Biakato.

Katika maandamano hayo magari manne yalichomwa moto pamoja na majengo kadhaa yaliteketezwa.

Maofisa wakuu wa shirika hilo akiwamo Mkurugenzi Mkuu, Tedros Adhanom, Ghebreyesus wamelaani shambulio hilo lililosababisha vifo na majeruhi. **BBC**



Wanaharakati wakipinga mauaji ya maofisa wa kukabiliana na ebola katika eneo la Ituri. **PICHA: BBC**

# Waandamanaji Iraq wachoma ubalozi wa Iran

**BAGHDAD,** Iraq

WAANDAMANAJI nchini Iraq wamevamia jengo la ubalozi mdogo wa Iran katika mji wa Najaf ambao ni mtakatifu kwa Waislamu wa madhehebu ya Kishia, kulichoma moto na kuliteketeza.

Wakati jengo hilo likivamiwa, wafanyakazi walikuwa tayari wameondolewa.

Maofisa wa usalama waliingilia kati kuutawanya umati wa waandamanaji kwa kutumia gesi ya kutoa machozi, na kwa mujibu wa watu walioshuhudia, watu wawili walipoteza maisha katika purukushani hizo.

Tangu mwezi Oktoba, maelfu ya Wairaq wanaandamana mitaani dhidi ya tabaka la wanasiasa wa nchi hiyo ambao wanawalaumu kwa kukithiri kwa ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka.

Katikia wiki za hivi karibuni, waandamanaji hao wamesikika wakiituhumu nchi jirani ya Iran kuunga mkono serikali ya Baghdad. **DW**

# Trump atia saini muswada kuwa sheria

**WASHINGTONG DC,** Marekani

RAIS wa Marekani Donald Trump, ameisaini sheria iliyopitishwa na Bunge la nchi hiyo, inayounga mkono vuguvugu la demokrasia mjini Hong Kong.

Sheria hiyo inaruhusu vikwazo dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu na inapiga marufuku mauzo ya vifaa vya kuzuia ghasia kwa polisi ya Hong Kong, kama vile gesi ya kutoa machozi, maji ya kuwasha mwilini, risasi ya mpira na vifaa maalum vinavyomfanya mlengwa kupoteza nguvu mwilini.



Akisaini sheria hiyo, Rais Trump alisema ana matumaini kuwa wawakilishi wa China na wanaharakati mjini Hong Kong wanaweza kumaliza tofauti zao kwa njia ya mazungumzo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Lee Yucheng, ameilaani hatua hiyo, akisema ni uingiliaji katika mambo ya ndani ya nchi yake. **DW**

# Rais Brazil ahukumiwa kwenda jela miaka 17

**BRAZILIA,** Brazil

MAHAKAMA ya rufani nchini Brazil imethibitisha hatia ya ubadhirifu dhidi ya rais wa zamani wa nchi hiyo, Luiz Inacio da Silva na kuongeza muda wa kifungo alichokuwa amehukumiwa cha miaka minne hadi miaka 17 na mwezi mmoja gerezani.



Rais huyo wa zamani anashutumiwa kutoa upendeleo kwa kampuni za ujenzi kupata zabuni za serikali, ambayo ilimsaidia kuikarabati nyumba yake ya kijijini alipokuwa madarakani.

Kiongozi huyo anazikanusha shutuma hizo, akisema zina malengo ya kisiasa. Lula da Silva aliachiwa kutoka gerezani wiki tatu zilizopita, kwa sababu bado anayo nafasi ya kukata rufani dhidi ya hukumu hiyo. **DW**

# Sirro awageukia wanaume wapinga madawati ya jinsia

**Na Mwandishi Wetu,** MARA

BAADHI ya wakazi wa Butiama mkoani Mara wameiomba serikali kuongeza nguvu kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ili kutokomeza tatizo hilo ambalo limeonekana kuwa sugu mkoani hapo huku baadhi ya wanaume wakidai ufunguzi wa madawati hayo utavunja ndoa kwa madai wanawake kuwa jeuri.

Walitoa ombi hilo wilayani Butiama baada ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, (IGP) Simon Sirro, kufungua ofisi ya dawati la jinsia na kwa nyakati tofauti wakazi hao kudai licha ya madawati ya jinsia kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili, lakini pia wanawake wamekuwa wajeuri kwa kuwa wanajua wataenda kushtaki.

Akizungumza na wananchi hao IGP Sirro, alisema mfumo dume bado unasumbua wanaume wa Mkoa wa Mara na kwamba jeshi la polisi haliwezi kuvumilia mambo yaliyopitwa na wakati hivyo, lazima washugulikiwe kwa nguvu zote.

"Salamu zangu kwa wanaume ubabe haulipi wakati Rais Magufuli akiniteua alikuwa na maana yake huwa nikisema jambo sitanii, sasa wewe baba jaribu uone," alisema Sirro.

Alisema mtu hana nafasi ya kuruhusu ukatili kwa mwanamke kwa sababu alitolewa mahari ya ng'ombe na ndiyo maana madawati yameanzishwa nchi nzima kulinda haki za wanawake na watoto, kuwataka wanawake wasizidi kusababisha balaa.

"Kinamama lindeni watoto wenu, wazazi wangu wasingenilinda leo nisingekuwa IGP, hujui mtoto wako atakuwa nani baadaye na nyie kinababa msiwarubuni watoto nendeni kwa wakubwa wenu wamejaa tele na nyie watoto wa kike msikubali kurubuniwa na vitu vidogo vikaharibu ndoto yako ukiona kuna viashiria vya mtu mzima kukurubuni au kukutaka kimapenzi nenda kwenye dawati," alisisitiza.

Naye Mkurugenzi wa jukwaa la utu wa mtoto, Koshuma Mtengeti, amesema kutokomeza ukatili wa jinsia kutaleta maendeleo kwa kuwa wanawake watajishughulisha kikamilifu kujenga uchumi na kuwa uzinduzi wa dawati hilo utatoa chachu kukusanya rasilimali na kuweka nguvu pamoja kutokomeza ukatili.

"Tunapata faraja sana kuona IGP anaongoza mapambano kutokomeza ukatili namini tutashinda cha msingi wananchi tutoe ushahidi pale unapohitajika hili ni janga letu sote," alisema Mtengeti.

Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (Unfpa), Jackqueline Mahon, alisema lengo ni ifikapo mwaka 2030 vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia viwe vimetokomezwa.

Pia ameipongeza Serikali ya Tanzania na Jeshi la Polisi kwa jitihada za kuhakikisha vitendo vya ukatili kwa wanawake na



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wakijitolea damu katika zoezi lililoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia wenye mahitaji kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama. Kulia ni Muuguzi kutoka Damu Salama, Peter Chami. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani mbogo wizi taa barabarani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MADIWANI wa Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, wameelezea kusikitishwa na vitendo vya baadhi ya watu kuharibu taa za barabarani ambazo zimewekwa hivi karibuni kwenye barabara zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami zenye urefu kilomita 10.3.

Walieleza hayo jana wakati wa kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo.

Diwani wa Ndilimalimbo, Crescensia Kapinga, alisema serikali imejitahidi kuweka miundombinu mizuri ya barabara za lami na kando ya barabara hizo zimewekwa taa ambazo zinatumia umeme jua lakini cha kushangaza baadhi ya watu wasiofahamika wamekuwa wakipanda kwenye nguzo na kung`oa taa ambazo zilishawekwa.

Alisema kwenye barabara ya kutoka makutano ya Mahenge kwenda idara ya maji, zimeng'olewa taa tatu na maeneo mengine haijafahamika ngapi zimeng'olewa, hivyo akaiomba serikali kupitia vyombo vya ulinzi kuona umuhimu wa kuweka mikakati endelevu ya kuhakikisha miundombinu hiyo inalindwa.

Diwani wa Bombambili, Golden Sanga, aliomba Wakala wa Barabara (Tanroads) kuona umuhimu wa kuweka taa za barabarani kwenye barabara kuu toka shule ya Tanga hadi Likuyufusi ili kuweka uwiano mzuri kwa kuwa mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 10.3 ndio umeweka taa za barabrani ndani ya manispaa.

Odo Mbunda, Diwani wa Mjimwema, alisema kwa muda mrefu kumekuwa na wafanyabiashara ambao wanafanya biashara zao katika maeneo ambayo hayaruhusiwi wakati halmashauri ya manispaa imetenga maeneo.

Alisema manispaa imejenga masoko likiwamo la mjimwema na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa, hivyo ni vyema idara ya mipango miji ikajipanga vizuri kuhakikisha maeneo yote ya biashara yanapaswa yawekwe na watu wanaotaka kufanya biashara wapewe vibali badala ya kufanya biashara holela.

Kwa upande wake, Diwani wa Viti Maalumu, Happyness Haule, aliuonya uongozi wa kituo cha Afya cha Mjimwema kutokana na uhaba wa maji, hivyo kutaka kuchukuliwa hatua za haraka ili kuondoa kero hiyo inayowakabili wagonjwa.

Meya wa Manispaa ya Songea, Alhaji Abdul Mshaweji, akijibu hoja za madiwani alisema zinafanyiwa kazi na tatizo la watu wasiojulikana kuiba taa za barabarani ataliwakilisha kwa mkuu wa mkoa ili kuona ni namna gani ya kuwabaini wahalifu hao.

# Uhaba mkubwa madarasa Rukwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKOA wa Rukwa unakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 2,888 hatua ambayo huenda ikasababisha wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwakani kukosa nafasi.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, ameziagiza halmashauri kuhakikisha zinakamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo ili kusiwapo mtoto atakayekosa nafasi.

Wangabo alitoa agizo hilo jana wakati akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) katika mwaka wa fedha 2019/2020 kilichofanyika katika ukumbi wa ofisi ya mkuu wa mkoa, mjini hapa.

Alisema wanafunzi waliofaulu darasa la saba mwaka 2019 ni 16,069 wakiwamo wavulana 7,953 na wasichana ni 8,116 wakati nafasi zilizopo ni 13,128.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wanafunzi ambao watakosa nafasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ni 361, Nkasi 1554, Manispaa ya Sumbawanga 179 na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni 794.

Kutokana na takwimu hizo, Halmashauri ya Nkasi inaongoza kwa kuwa na wanafunzi wengi watakaokosa nafasi ikifuatiwa na Halmashauri ya Sumbawanga, Kalambo na Manispaa ya Sumbawanga.

Wangabo aliwaagiza wakuu wa wilaya kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanajiunga kidato cha kwanza ifikapo Januari, mwakani na kuwa hakutakuwa na udahili wa pili kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum, Silafi Maufi, alishauri kuwapo na kawaida ya kuwapima mimba wanafunzi mara kwa mara kuliko kusubiri mpaka wahisiwe kuwa na ujauzito.

Pia alishauri kuwa wanaume waliosababisha mimba hizo wakamatwe na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria mara moja.

Mkoa wa Rukwa una wanafunzi 294 waliokatisha masomo kutokana na kupata ujauzito katika kipindi cha mwaka huu.

**Wanafunzi waliofaulu darasa la saba mwaka 2019 ni 16,069 wakiwamo wavulana 7,953 na wasichana ni 8,116 wakati nafasi zilizopo ni 13,128.**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

KIWANJA KINAUZWA

KIPO CHANIKA BUYUNI PLOT 256, SQM 947 BLOCK 14. HATI IPO BEI NI SHILINGI MILIONI 14. KWA MAWASILIANO: 0743 113 138 / 0757 305 222.

## KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA CHATO**

**MAHALI LILIPO CHATO**

**MAOMBI/RUFAA NA. 19 MWAKA 2019**

**ELIZABETH MUSA................MWOMBAJI/MRUFANI**

**DHIDI YA**

**SABINI MAFUSO & GILSON EMMANUEL...............MJIBU MAOMBI/MRUFANIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA:** 1. **SABINI MAFUSO**
2. **GILSON EMMANUEL**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 3 mwezi Desemba mwaka 2019 saa 2:30 asubuhi mbele ya **MH. BAHATI COLEX NDAMBO** Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa pamoja na utetezi/majibu yako ndani ya siku 21.

**AMRI** hii imetotolewa leo kwa mkono wangu na Lakiri/Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 18th mwezi Novemba mwaka 2019.

115537902

PROSHARE CAPITAL LTD

**TANGAZO LA MAGARI YANAUZWA;**


BARAKA A. JEREMIAH
**AUDI T 576 DKV**

FAKIHI H. GELENTE
TOYOTA NOAH
T 394 CZM

FATUMA K. MBWEGO
T 395 DQJ

115537201

## KUPOTEA KWA CHETI



**DENNIS M. MHEZA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.4692-0575** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. JOSEPH'S CATHEDRAL HIGH SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/414235/2019.**

115537002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NWAKAEGO EUCHARIA UZOKWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 895 BZC NISSAN X-TRAIL.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/507163/2019.**

115537102

## KUPOTEA KWA CHETI



**Araphat R. Mbwana** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Enyoito chenye **index No S. 1125-0148** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2016.Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **MOS/RB/1732/19**

115536602


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ERIKSEN KUONDOKA SPURS JANUARI

**LONDON,** England

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen, anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo itakapofika Januari mwakani baada ya kupata dili mbili mpya.

Kwa mujibu wa Corriere Dello Sports limeripoti kwamba, Eriksen yupo mguu mmoja nje, mwingine ndani katika klabu hiyo baada ya kushindikana kusaini mkataba mpya na anataka kutumia dirisha la uhamisho wa Januari kuondoka.

Kiungo huyo amebakiza miezi sita kwenye mkataba wake, huku Juventus na Real Madrid zinatajwa kumtolea macho akakipige kwenye vikosi vyao.

Kocha wa Tottenham, Jose Mourinho, ameweka wazi kwamba alishazungumza na Eriksen kuhusu hatima yake na alisema kwamba kiungo huyo ataendelea kusalia katika kikosi hicho kwa asilimia 100.

Kiungo huyo amekuwa akihusishwa mara kwa mara kuondoka katika klabu hiyo lakini amekuwa akiendelea kusalia baada ya kushindwa kuhama kwenye dirisha lililopita la uhamisho wa majira ya kiangazi huko Ulaya.

# Pochettino njia nyeupe Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich wameonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumtwaa aliyekuwa Kocha wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, mabosi wa Bayern Munich wamepanga kukutana na Pochettino kujadili mpango wa kumpa timu japo anaweza kukutana na upinzani kutoka kwa Erik ten Hag, ambaye anainoa Ajax kwa sasa.

Hata hivyo, kabla ya mabosi hao wa Bayern kumuita Pochettino mezani kujadili mpango huo, kikao cha mabosi kitakaa ili kupata mwafaka wa pamoja na kuwajadili makocha ambao, wangependa mmoja wao atue Bavarian.

Pochettino, ambaye ametimuliwa kazi wiki iliyopita na Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, kwa sasa amekuwa akiwindwa na vigogo vya soka Ulaya ikiwamo Real Madrid, Manchester United na Arsenal.

Nafasi yake baada ya kufutwa kazi imechukuliwa na kocha wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, ambaye alianza vema kibarua chake akiipa ushindi wa kwanza Spurs ugenini dhidi ya West Ham United.

Kwa sasa Bayern iko chini ya kocha wa muda, Hans-Dieter Flick, ambaye ameshinda mechi tatu mfululizo huku akikusanya mabao 10 ya kufunga bila kuruhusu wavu wake kutikiswa, baada ya kufutwa kazi kwa Niko Kovac.





# *Lampard awatia ndimu wachezaji*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema kuwa wachezaji wake wanatakiwa kupambana kila wanapocheza na timu zilizo nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

"Kama tunahitaji kutwaa ubingwa au kufanya vizuri kwenye ligi lazima tukubali kupambana na Liverpool, Tottenham Hotspurs, Manchester City na timu nyingine zote kubwa.

"Wachezaji wangu wanapaswa kupambana sana kila wanapocheza na hizi timu sita za juu," alisema Lampard.

Chelsea ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi zake 26 nyuma ya pointi 11 ya Liverpool waliopo kileleni.

Timu hiyo ilichapwa mabao 2-1 na Manchester City mchezo wa Ligi Kuu England uliopigwa kwenye Uwanja wa Etihad.

## HABARI MICHEZO

# Bayern bado wamkomalia Leroy Sane

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imeanzisha tena mazungumzo ya kutaka kumwania winga wa Manchester City, Leroy Sane.

Kwa mujibu wa ESPN tayari viongozi wa Bayern wamekutana na wakala wa staa huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Giovanni Branchini, kwa ajili ya kujadili uhamisho huo.

Kwa sasa Sane ni majeruhi na Bayern haitazamiwi kumchukua katika dirisha la Januari mwakani, lakini inatazamiwa kutoa dau katika dirisha kubwa la majira ya joto, huku City wakitaka zaidi ya pauni milioni 100 kumruhusu nyota huyo kuondoka.

Hii ni mara ya pili kwa Bayern kurudi kwa Sane baada ya kumsaka kwa nguvu zote katika dirisha kubwa lililopita la majira ya joto kwa ajili ya kuziba mapengo ya wakongwe wao waliotimka klabuni hapo.

Arjen Robben na Franck Ribery tayari waliondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu uliopita.

Sane ameifungia City mabao 25 baada ya kuichezea mechi 89 timu hiyo hadi sasa.







# MADRID WAZIDI KUMNYATIA MBAPPE

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anawaza namna ya kumsajili nyota wa klabu ya Paris Saint German, Kylian Mbappe.

Zinade na mabosi wake pale Real Madrid kwa nyakati tofauti wamekuwa wakimfuatilia Mbappe akifanya yao uwanjani kisha kufanya uamuzi mgumu wa kuvunja benki na kupata huduma yake.

Eden Hazard ambaye ametua hapo Madrid akitokea kule Chelsea amefichua kuwa Mbappe ni mchezaji mzuri na kiwango chake kimekuwa kikiimarika kila kukicha na kwamba, yuko tayari kusaidia kumleta Santiago Bernabeu.

Madrid ambayo ilitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na PSG, katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu Jumanne, akili yao inamtaka kwa udi na uvumba mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Licha ya uwepo wa Neymar Jr, Mauro Icard na Di Maria kwenye kikosi cha PSG, lakini tahadhari kubwa imewekwa kwa Mbappe kutokana na kasi yake katika kufumania nyavu.

Katika mchezo wa kwanza uliofanyika jijini Paris, Ufaransa Real Madrid ilichapwa mabao 3-0 kisha ikalazimisha sare na Club Brugge na kupata ushindi.

PSG iliingia mchezo huo ikiwa tayari imeshatinga hatua ya 16 bora, ikishinda mechi nne dhidi ya Madrid, Galatasaray na Brugge na kuvuna alama 12 ikiwa kileleni mwa msimamo, kabla ya kupata sare hiyo na kufikisha pointi 13.



# *Arsenal yahofia kumtimua Emery*

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal wamechelewesha kumfuta kazi, Unai Emery kabla ya msimu kumalizika wakikwepa kulipa fidia ya pauni milioni 4, kwa mujibu wa ESPN FC.

Raia huyo wa Hispania yupo kwenye presha kubwa pale kwenye uwanja wa Emirates baada ya timu hiyo kufanya vibaya na hawajashinda mechi yoyote tangu Oktoba 24, huku Oktoba 6 mwaka huu, ndiyo ilikuwa mara ya mwisho kushinda kwenye Ligi Kuu England.

Sare dhidi ya Southampton Jumamosi iliyopita ilimweka kwenye wakati mgumu zaidi Emery, lakini Arsenal wanaogopa kumfukuza sababu tu hawataki kulipa fidia hiyo ya pauni milioni 4.

Inaelezwa kuwa wanasubiri ifike mwisho wa msimu ambapo, ataondoka bila ya kuwaingiza kwenye gharama yoyote ile.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## VIGOGO SABA ULAYA WAMGOMBEA HAVERTZ

●●● Ni baada ya Mjerumani huyo kuonyesha kiwango cha juu akiwa na Bayer Leverkusen...

**LEVERKUSEN,** Ujerumani

NYOTA wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz, anatajwa kuanza kufanya mazungumzo na klabu kubwa za Ulaya ambazo zinataka kumsajili katika dirisha la usajili la majira ya joto mwakani.

**Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 20 ameonyesha kiwango cha juu msimu huu kwenye Bundesliga tangu alipopandishwa katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo mwaka 2017, na msimu uliopita alifunga mabao 17 kwenye ligi hiyo ya juu nchini Ujerumani.**

Na kutokana na uwezo aliouonyesha, mwaka jana kwa mara ya kwanza, Havertz alijumuishwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ujerumani.

Klabu za Manchester United, Liverpool, Real Madrid, Chelsea, Manchester City, Bayern Munich na Barcelona zimetajwa kuanza mazungumzo na wakala wake kwa ajili ya kuwania saini yake, gazeti la Bild la Ujerumani limeandika.

Imeandikwa kuwa huenda mchakato wa uhamisho wa Mjerumani huyo ukafanyika katika dirisha la usajili la Januari, lakini Havertz anataka kuona anaendelea kuitumikia klabu hiyo ya Bundesliga hadi mwishoni mwa msimu na majira ya joto mwakani ndio akajiunga na timu nyingine.

Kiungo huyo anaamini akibakia klabu hapo, atapata nafasi nzuri ya kuimarisha kiwango chake na kumvutia Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low ili kumjumuisha kwenye kikosi chake kitakachoshiriki katika mashindano ya Kombe la Euro 2020.

Bayern Munich ambayo ilitoa ofa ya pauni milioni 76 katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, ilishindwa kumnasa Havertz, ambaye sasa thamani yake imepanda na kufikia pauni milioni 110.

Nyota huyo amekaririwa akisema kuwa anatarajia kufikia uamuzi kuhusu hatima yake ndani ya siku chache zijazo na anataka kuona anafanya kazi na kocha ambaye anamwamini, na kumtaja kama Mauricio Pochettino.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp naye ameeleza namna anavyohitaji kufanya kazi na kiungo huyo, sambamba na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

"Nafikiri nimeshapata uzoefu wa kutosha wa kushiriki mashindano ya kimataifa nikiwa hapa Leverkusen," alisema Havertz.

"Nimeshajua ushindani na namna ya kupambana kwenye mechi za kimataifa, na sasa ninajiamini ninaweza kwenda kucheza katika klabu yoyote nje ya Ujerumani. Kwa sasa ninataka kuona ninakuwa na msimu mzuri, baada ya hapo tutafahamu," aliongeza kiungo huyo.

## ZISIKUPITE

### MOURINHO AMTAKA TOBY

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anaamini beki wake mwingine wa anayeichezea Timu ya Taifa Ubelgiji, Toby Alderweireld (30), atasaini mkataba mpya na klabu hiyo hivi karibuni. ***(Football.London)***

### VIEIRA KUTUA MIAMI

DAVID Beckham amemweka katika nafasi ya kwanza, kiungo wa zamani wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Patrick Vieira, kutua kwenye klabu Inter Miami. ***(Telegraph)***

### SANCHO AIKATAA UNITED

WINGA wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19), anaamini kwamba anastahili kujiunga na Real Madrid au Barcelona na si Manchester United au Liverpool. ***(Star)***

### MOYES KUREJEA WEST HAM

WEST Ham inatarajia kufanya mchakato wa kumrejesha aliyekuwa kocha wake, David Moyes, kama itafikia uamuzi wa kumfukuza, Manuel Pellegrini. ***(London Evening Standard)***

### GUARDIOLA APEWA RUNGU

PEP Guardiola anatarajiwa kuendelea kupewa nguvu zaidi katika kukiongoza kikosi cha Manchester City ili kuifanya klabu hiyo iwe imara zaidi, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Khaldoon Al Mubarak, amesema. ***(Goal.com)***

### DEFOE AJIWEKA PAZURI

STRAIKA wa zamani wa England ambaye anaichezea Rangers kwa mkopo, Jermain Defoe (37), amesema yuko tayari kutolipwa ada ili akamilishe mchakato wa kupata mkataba wa kudumu kwenye klabu hiyo, akitokea Bournemouth. ***(Football Insider)***

### FERNANDES AJIFUNGA LISBON

NYOTA aliyekuwa anawindwa na Manchester United na Tottenham, Bruno Fernandes, ambaye ni kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, amesaini mkataba mpya wa klabu yake ya Sporting Lisbon ambapo sasa thamani ya kuvunja mkataba huo imepanda kutoka pauni milioni 20 hadi pauni milioni 85. ***(Mirror)***

### UMTITI KUONDOKA BARCA

BEKI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Samuel Umtiti (26), ambaye amekosa namba kwenye kikosi cha klabu hiyo amesema alipenda kuona anastaafu soka akiwa kwenye timu hiyo, lakini analazimika kusaka klabu nyingine ya kuichezea ili awe kwenye kikosi cha kwanza. ***(Sport)***

### CELTIC WAMTOA KOUASSI

MABOSI wa Celtic wamesema wako tayari kuona kiungo wake raia wa Ivory Coast, Eboue Kouassi (21), anaondoka klabuni hapo au anapata klabu nyingine ya kuitumikia kwa mkopo katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Football Insider)***

### VERTONGHEN ASUBIRI

BEKI wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen (32), ataendelea kusubiri kuhusu uamuzi wa Tottenham kumpa mkataba mpya kufuatia kuwasili kwa kocha mpya, Jose Mourinho kwenye klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

## Matola atajwa kurejea Simba

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEWAHI kuwa Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, ambaye kwa sasa anakiongoza kikosi cha Polisi Tanzania, anatajwa kurejea kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Kwa mujibu wa chanzo chetu, mazungumzo kati ya mabosi wa Simba na nahodha huyo wa zamani wa Simba, Matola, yameshafanyika.

Chanzo chetu kilisema kuwa Matola anatarajiwa kutua Simba ili kuchukua mikoba ya Dennis Kitambi, ambaye kwa sasa anaiongoza timu baada ya Kocha Mkuu, Patrick Aussems, kusimamishwa kwa muda.

"Matola anatarajiwa kutangazwa kuwa kocha msaidizi wa Simba, tayari mazungumzo yamefanyika na ataungana na kocha mpya atakayekuja," kilisema chanzo chetu.

Wakati huo huo, Bodi ya Wakurugenzi ya Simba ilikutana na Aussems, katika kikao ambacho kinaelezwa kuwa na mvutano katika pande hizo mbili.

"Leo (jana) Bodi ya Wakurugenzi ilikutana na kocha mkuu ili waweze kutoa uamuzi wa pamoja na itawajulisha rasmi mashabiki wa Simba na Watanzania, ilichokiamua," kilisema chanzo hicho.

Baada ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Chalenji, vinara wa ligi hiyo, Simba watashuka tena dimbani Desemba 30, mwaka huu kuwakabili Ndanda FC ya Mtwara.

## Mshindi wa gofu kuzawadiwa gari

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa gofu 150 kutoka katika nchi sita barani Afrika wanatarajia kuchuana katika mashindano ya wazi yanayotarajiwa kufanyika leo kwenye Uwanja wa Kili jijini Arusha, imeelezwa.

Mashindano hayo yatashirikisha wachezaji kutoka Kenya, Uganda, Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda na wenyeji Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Chriss Martin, alisema kuwa maandalizi kuelekea mashindano hayo yamekamilika na kinachosubiriwa ni wanamichezo kuanza kuchuana kuwania zawadi mbalimbali ikiwamo gari.

"Tuna zawadi nono na kubwa zaidi ni gari aina ya Rav 4 ambayo itakwenda kwa mchezaji atakayefanikiwa kupiga mpira mmoja na kuingiza shimoni moja kwa moja," alisema Martin.

Naye mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Mashindano, Kapteni, Japhet Masai, alisema kuwa sheria zitakazotumika katika michuano hiyo ni za kitaifa ambazo zimeainishwa kwenye karatasi ya kuandikia matokeo sambamba na sheria za kimataifa.

Masai alizitaja klabu za Tanzania zitakazoshiriki mashindano hayo yanayodhaminiwa na Oryx, Super Doll, Garda word, Coca Cola, Tanfoam na Serengeti ni Lugalo, Gymkhana (Dar es Salaam, Morogoro na Arusha), Mufindi na Zanzibar Sea Cliff.

# YANGA, KOCHA ZAHERA KUMALIZANA JUMATATU

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), anatarajia kukutana na viongozi wa klabu hiyo Jumatatu ili kufahamu hatima ya fedha ambazo aliikopesha wakati akiiongoza timu hiyo, imelezwa.

**Zahera ambaye alitua nchini kurithi mikoba iliyoachwa na Mzambia George Lwandamina, alitua nchini juzi kwa lengo la kumalizana na klabu hiyo ambayo leo itakutana na Alliance FC, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.**

Yanga iliamua kuachana na kocha huyo bila kutaja sababu, baada ya timu yao kuondolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, na sasa inanolewa na Boniface Mkwasa. Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Zahera, alisema kuwa anaidai Yanga kiasi kikubwa cha fedha (hakutaka kutaja deni halisi), na safari yake ya kurejea nchini ni kuhakikisha analipwa fedha hizo.

Zahera alisema kuwa tayari ameshauandikia uongozi wa Yanga, barua inayoeleza kiasi cha fedha anachowadai, kama ambavyo wamemtaka afanye hivyo.

"Mimi nimekuja kwa ajili ya kuchukua fedha zangu ambazo ninaidai Yanga, viongozi wameniambia nisubiri mpaka Jumatatu, kwa sababu Ijumaa (leo), wana mchezo na timu ya Alliance huko Mwanza," alisema Zahera.

Kocha huyo alisema kuwa fedha hizo anazodai, ni zile ambazo alikuwa akiwakopesha ili kulipia huduma mbalimbali za timu wakiwa kwenye mechi za Ligi Kuu Bara au za mashindano ya kimataifa waliyokuwa wanashiriki msimu huu.

"Unajua kuna fedha ambazo mimi nilikuwa nazitoa kwa ajili ya timu, ambazo viongozi ndio walitakiwa wazitoe, lakini nilikuwa nafanya ili mradi timu ikae vizuri, na tulikubaliana watanilipa," alisema Zahera.

Hata hivyo, Zahera, alisema kuna fedha nyingine alikuwa akitoa na kuwapa wachezaji kutokana na kufanya vizuri, hizo hajazijumlisha kwenye madai aliyoyawasilisha kwa viongozi.

Kocha huyo alisema pia, kwa sasa bado yuko huru, kutokana na kutopata ofa ya klabu yoyote inayomhitaji.



Kocha wa mchezo wa tenisi, Riziki Salum (kushoto), akipiga mpira kuwafundisha wachezaji wa timu ya wenye ulemavu ya Tanzania, ambao wanajiandaa na mashindano ya wazi ya Kenya yanayotarajiwa kufanyika mwezi ujao nchini humo. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Mkutano Mkuu Taswa Desemba

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO Mkuu Maalum wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (Taswa), unatarajiwa kufanyika Desemba 29 mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Taswa, Amir Mhando, alisema jana kuwa lengo la mkutano huo ni kujadili masuala mbalimbali ya chama hicho, ambapo pia utapokea taarifa kutoka Kamati ya Marekebisho ya Katiba iliyoundwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Mhando alisema pia wanatarajia kupokea mapendekezo ya katiba kutoka Kamati ya Utendaji ya chama hicho inayomaliza muda wake.

Aliwataja wanachama watakaohudhuria mkutano huo ni wanachama wote walio katika leja baada ya kushiriki uchaguzi wowote wa chama hicho kuanzia mwaka 2004, 2007, 2010, 2014 na wanachama wapya wote waliongia kuanzia mwaka 2015 hadi Juni mwaka huu.

"Ili mkutano ufanyike kwa ufanisi, ni vyema mwanachama yeyote mwenye nia ya kushiriki athibitishe kwa maandishi akitaja jina lake na chombo anachofanyia kazi na kutuma kwa email: taswatz@yahoo.com au mgosius@yahoo.com kwa wanachama wa zamani, wakati wanachama wapya uratibu utasimamiwa na mwandishi, Gift Macha na watume kwa email: machagift@gmail.com, ili taratibu nyingine zifanyike. Mwisho wa kuthibitisha ushiriki ni Desemba 10 mwaka huu," alisema Mhando.

Aliwataka pia wanachama hai wa chama hicho, kujiunga na Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo cha Kimataifa (AIPS) chenye makao yake makuu Lausanne, Uswisi ili kupata fursa za kufanya kazi katika mazingira mbalimbali ya michezo duniani.

# Michezo

Ijumaa Novemba 29, 2019

Nipashe




Vigogo 7 Ulaya wamgombea Havertz

UKURASA 30



Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah (kushoto), akiwania mpira na beki wa Napoli, Mario Rui, katika mechi ya Kundi E ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield juzi usiku, Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAJIPANGA KUENDELEZA DOZI

## ●●● Hata hivyo Mkwasa afunguka kuwa kikosi chake kitacheza kwa tahadhari na umakini...

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU ikiendelea kukosa huduma ya beki wake wa kati, Andrew Vicent "Dante", ambaye anaidai fedha za usajili klabu hiyo, Yanga inatarajia kuwavaa wenyeji wao, Alliance FC katika mechi ya "kiporo" ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

**Yanga itashuka katika mchezo wa leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-2 iliyoupata dhidi ya JKT Tanzania, wakati Alliance wao, walichapwa mabao 5-0 na Azam FC kutoka jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, alisema kuwa kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo ambao wanatarajia kucheza kwa tahadhari ili kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu muhimu.

Mkwasa alisema kuwa wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo, na kuwataka wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza, kutowadharau wapinzani wao.

Kocha huyo alisema kuwa wanaamini matokeo ya ushindi ndiyo yatawasaidia kuendelea na mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na wapinzani wao, Simba, ambao kwa sasa ndio wako kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

"Tunatarajia kuwa mchezo wa kesho (leo), utakuwa mgumu na wenye ushindani, tunatarajia kucheza kwa tahadhari kubwa, tunahitaji kupata matokeo chanya," alisema kocha huyo.

Alisema pia anatarajia kuona wapinzani wao wakibadilisha aina ya mchezo waliouzoea kwa sababu ya kuhitaji kupata matokeo mazuri, jambo ambalo tayari amewaandaa wachezaji wake kukutana na hali hiyo.

Kessy Mziray, Kocha Mkuu wa Alliance FC, alisema kuwa anatarajia mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu wao wanahitaji kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwenye mechi iliyopita, huku Yanga ikijipanga kuendeleza wimbi la ushindi. Mziray alisema kuwa wachezaji wake wote wako katika hali nzuri, na wameahidi kucheza kwa utulivu ili wasipoteze pointi.

"Hatutarudia makosa, tumeangalia pale tulipokosea katika mchezo wetu uliopita, ninaamini tutaingia uwanjani kesho (leo) Ijumaa tukiwa tofauti, kila mchezaji ameahidi kupambana ili kuipa timu heshima," Mziray alisema.

Alimtaja mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Jerry Tegete na Daudi Richard, ndio wanatarajia kuongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa pili.

Yanga ambayo imecheza mechi sita, ina pointi 13 wakati Alliance FC ambao wameshuka dimbani mara 12 wamejikusanyia pointi 17.

# Mwakinyo atamba kummaliza Mfilipino

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, amesema kuwa amejiandaa kulinda heshima ya Tanzania kwa kumdunda mpinzani wake, Arnel Tinampay, kutoka Filipino katika pambano litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Mgeni rasmi katika pambano hilo la raundi 10, uzito wa Super Welter, anatarajiwa kuwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwakinyo (pichani chini), alisema kuwa amefanya mazoezi kwa muda mrefu na sasa ni wakati wa kuonyesha matunda ya kile alichokuwa anakifanya kuelekea pambano hilo.

Mwakinyo alisema kuwa amejiandaa kulinda heshima ya nchi kwa kutokubali kupoteza pambano hilo, ambalo anaamini litakuwa na ushindani, kutokana na rekodi za mabondia wote wawili.

"Nimejiandaa kufanya vizuri pambano hili, nimejipanga kuendeleza rekodi yangu ya kushinda kwa KO, nataka kulinda heshima ya nchi yangu, ninatarajia kuendeleza ndoto za kufanya vema katika kila pambano," alisema Mwakinyo.

Bondia huyo alisema kuwa amejipanga kutowaangusha Watanzania wenzake kwa sababu, hilo ni pambano lake la kwanza kubwa kucheza hapa nyumbani.

"Sitaki kusema sana, kwa sababu ya namna nilivyojiandaa, lakini ninaamini hawezi kumaliza raundi ya 10," aliongeza bondia huyo kutoka jijini Tanga.

Naye Tinampay, alisema kuwa amejiandaa vema kwa pambano hilo na amekuwa akimfuatilia Mwakinyo, katika mapambano mbalimbali ambayo amecheza.

"Nimejiandaa kushinda, sihofii mashabiki wengi wa Mwakinyo, hii ni kawaida unapopigana ugenini," alisema Mfilipino huyo.

Naye Mratibu wa pambano hilo, Anthony Lutta, amesema kuwa maandalizi yamekamilika na anaamini Watanzania watajitokeza kumshangilia bondia wao ili atimize malengo ya kumchapa mpinzani wake.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042